Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 77 No. 193 | Jum I - Jum. II 1439 AH | FEBRUARI 2018 | TABLIGH 1397 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

"Na waja wangu wakuulizapo juu Yangu, basi hakika Mimi Nipo karibu. Nayaitika maombi ya mwombaji anaponiomba, basi waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka." (2:187).

Khalifatul Masih V a.t.b.a afafanua

Falsafa ya Maombi katika Islam

Na Mwandishi Wetu

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 16/02/2018, Hadhrat Amir-ul Muminiin, Khalifatul Masih Va.t.b.a.alizungumziajuu ya Nguvu ya Maombi ya Dhati.

Baada ya Tashahhud, Taa'udh na Surat Fatihah Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Safari moja Hadhrat Masihi Mauud as akielezea falsafa ya maombi alisema ya kwamba wakati mtoto mchanga akishikwa na njaa kali anapolilia maziwa, basi ghafla maziwa huteremka matitini mwa mama. Mtoto huyo hana habari ya maombi hata kidogo lakini kivipi kulia kwake kunayasababisha maziwa yatoke, alisema ya kwamba wakati mwingine imeonekana ya kuwa mama anakuwa hajisikii uwepo wa maziwa matitini mwake lakini kilio cha mtoto huyavuta maziwa yatoke. Basi je vilio vyetu vitakavyokuwa mbele ya Mungu je havitaleta matokeo yoyote?

Matokeo hutokea na ni lazima yatokee lakini vipofu wa kiroho wanaojifanya kuwa wenye akili na busara wao hawawezi kuyashuhudia.

Mahusiano ambayo mtoto huwa nayo na mamaake, kwa kuyaweka mbele yake ikiwa binadamu atafakari juu ya falsafa ya dua basi atajisikia urahisi wa kumwomba Mungu.

Sisi Wanajumuiya tumebahatika kwa Fadhila Zake Allah ya kwamba wengi wetu walio wakubwa na wadogo huelewa kuwa ikiwa kwa unyenyekevu mkubwa na kwa kujitupa mbele ya Mungu maombi yafanywe basi Mwenyezi Mungu Huyasikiliza maombi na baadhi ya wakati matukio

Endelea uk. 3



Sehemu ya waumini ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London ambao Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. hutoa hotuba zake za Ijumaa na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Ukweli Kuhusu Ibilisi na Sheitwani

Mwl Abdullah H. Mbanga

Katika matoleo kadhaa yaliyopita ya Mapenzi ya Mungu sahibu yangu Sheikh Ahmad Daudi Mmoto alikuwa akitegua kitendawili cha Majini, kwa hakika makala yake ilivutia mnoo na ninatumai kwamba wale wote waliokuwa wanatizwa na kitendawili kile bila shaka walipambanukiwa. Kwakuwa kuna mada nyingi zinazokwaza watu katika maelezo ya Quran Tukufu, na mimi baada ya kujitafutia usahihi wa mada yenyewe nimeona bora nieleze uwazi kuhusu Ibilisi na Sheitwan mada ambayo pia ni miongoni mwa vitendawili kadhaa ambavyo waumini wa dini nyingi wanashindwa kuvitegua. Neno ibilisi linatokana na mzizi wa neno ABLASA, ambalo humaanisha 1) aliyepungukiwa na heri, 2) aliyepoteza matumaini na kukata tamaa na rehma za Mwenyezi Mungu, 3) Aliye vunjika moyo, 4) Aliye potea na kushindwa kuiona njia yake 5) Aliyezibwa mdomo kwa hoja, 6) Aliye shindwa kukidhi haja yake, n.k, na vile vile ibilisi huchukuliwa kuwa kama jina la sheitani. (LANE Arabia –English Dictionary). Kwa kuzingatia maana ya neno la Asili yaonekana kuwa Ibilisi ni yeyote mwenye ubaya zaidi kuliko wema. Kwani sifa kubwa ya Ibilisi ni kuasi amri na kwa hili ajijengea misingi ya kupotea njia iliyo nyooka . Ingawa Ibilisi huonekana kuwa ndiye sheitan, lakini baadhi ya nyakati huwa ni wahusika wawili tofauti. Utajo wa kwanza wa Ibilisi unaonekana katika Qur`an Tukufu ni ule uliopo katika Sura Al-Bakara ambayo Adam a.s baada ya kufundishwa majina ya Allah Malaika wanapewa amri ya kumtii (2:35) ndipo Malaika wote wakamtii isipokuwa Ibilisi ambaye alikuwa miongoni mwa makafiri. Hapa lazima ieleweke Vizuri kwamba Ibilisi hakuwa miongoni mwa Malaika, kwani wakati hapa Ibilisi anasemwa kuwa ni katika makafiri wasiomtii Mwenyezi Mungu, Malaika wanafanywa kuwa ni viumbe watiifu na wasioweza kumuasi Mungu.(66:7) na kwa hiyo Ibilisi hawezi kuwa Malaika. Haja ya kwamba kwa nini Allah Amkasirikie Ibilisi kwa kutotii ilihali Amri ya utii ilitolewa kwa Malaika na sio juu yake, hii haina msingi,

Endelea uk 4

Upepo wa Mabadiliko Wavuma Afrika

Kwa miaka twende miaka rudi habari kutoka Afrika zimekuwa ni zile zinazohusu njaa, mafuriko, vita na mauwaji. Tunamshukuru Allah ya kwamba katika miaka ya hivi karibuni tumewaacha vinywa wazi wale wote wanaoamini hakuna jema lolote linaloweza kutoka Afrika. Hivi karibuni taifa lililokuwa limekumbwa na machafuko limeonesha kuonyesha ukomavu wa kisiasa. Aliyekuwa Raisi wa Liberia Bi. Ellen Johnson Sirleaf kwa mshangao wa wengi alimuunga mkono mgombea wa upinzani. Kumbe upinzani si uadui. Ni kutofautiana fikra. Na hiyo ni rehema kwa nchi. Gabriel Mugabe aliwekwa pembeni kwa ustaarabu na taadhima. Isingekuwa vinginevyo. Alipambana kwa bunduki hadi taifa la Southern Rhodesia likawa Zimbwabwe. Mcheza kwao hutunzwa. Tusameheane na kusahau yaliyopita. Muhali kwenda mbele. Jacob Zuma baada ya mawimbi makali katika bahari ya siasa akaona apatikane nahodha mwingine. Na ikawa hivyo. Hiyo ni Afrika mpya. Hiyo ni Afrika inayotufanya kuona fahari kuwa wana Afrika. Mungu Ibariki Afrika.

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Buriani Kingunge Ngombale Mwiru

Wakati tunafanya matayarisho ya kuzindua kitabu cha Mathiasi Mnyampala kiitwacho "Maisha ya Hayati, Sheikh Kaluta Amri Abeid" tulipiga hodi katika ofisi za viongozi wengi, ili washiriki katika uzinduzi wa kitabu ambacho mwandishi ni mshairi maarufu wa nchi hii ambaye aliandika juu ya mshairi mwingine maarufu wa nchi hii.

Kamati hiyo ya uzinduzi wa kitabu hicho ilikuwa na viongozi maarufu wafuatao mwenyekiti akiwa Brigedia Jenerali mstaafu Hashim Mbita, ambaye katika kazi zake nyingi alizoifanyia Afrika ni pamoja na kuwa Katibu Mtendaji wa Kamati ya Ukombozi wa Afrika, mjumbe mwengine alikuwa ni Balozi Jaafar Msolomi ambaye aliwahi kuwa Balozi wetu nchini Guinea na Uingereza na kuwa katibu wa kwanza wa Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi, mjumbe mwingine alikuwa ni Suleiman Hegga mtangazaji maarufu wa redio aliyekuwa anaongoza kipindi cha "Mbinu za Kiswahili" Tumetaja majina yote hayo, kuonyesha ya kwamba kama hawa walipuuzwa ingekuwaje kwa akina "pangu pakavu weka mchuzi". Katika masikitiko yote hayo, aliyeipa faraja kamati hiyo baada ya kuzunguka sehemu zote hizo alikuwa ni ndugu Kingunge Ngombale Mwiru na ni vizuri kukumbuka ya kwamba Kingunge Ngombale Mwiru maana yake ni "Kisiki Haking'olewi kwa Macho" lazima ufanye shughuli. Hivyo kifo chake cha hivi karibuni, kimetugusa na kutukumbusha mengi, na yapo mambo ambayo tunaweza tukajifunza kutoka katika maisha yake.

Kingunge alionyesha ni kwa kiasi gani alikuwa anaheshimu utamaduni wetu, alifurahi sana alipopata mualiko huo kwani alisema ya kwamba, hawa mabingwa wawili Mathiasi Mnyapala na Kaluta Amri Abeid, walisaidia sana katika kuleta maendeleo ya Kiswahili chombo muhimu katika ukombozi wa nchi hii.

Juhudi za Kingunge Ngombale Mwiru za kuendeleza utamaduni wetu ni za siku nyingi tangu alipokuwa vijana (TANU Youth League) na Mkuu wa mkoa, zinakumbukwa na kuheshimiwa sana. Tunahitaji viongozi wanaoheshimu utamaduni wetu kama alivyokuwa Kingunge Ngombale Mwiru. Kingunge alikuwa pia miongoni mwa wanafunzi wa mwanzoni kupelekwa na chama cha Tanu kusoma huko Afrika ya Magharibi. Alipenda sana kusoma na kujiendeleza na alipenda sana kusoma vitabu mbalimbali. Tuna mawili ya kujifunza hapo. Kwanza ni kwamba vyama vya siasa visisubiri kuingia Ikulu ili kuwasomesha na kuwatayarisha viongozi wake, chama cha TANU katika hili kinastahili pongezi na heshima. Kwani hata michango ya chuo kikuu cha Dar es salaam, ilianza kabla TANU haijaingia madarakani. Kingunge Ngombale Mwiru, alikuwa na uwezo wa kujenga hoja. Kupayuka haikuwa hulka yake. Atakusikiliza mpaka mwisho, ndipo ajenge hoja. Sikuwahi kumsikia hata siku moja akitumia matusi. Hayo ni mambo ya msingi ambayo kizazi hiki kitafanya busara kuyachukua. Kingunge alisimamia kwa dhati yote aliyoyaamini na hakuficha imani yake. Kwa ufupi hakuwa kizabi zabina. Huo ni utamaduni mwengine mzuri ambao kizazi kipya kina mengi ya kujifunza kutoka kwa Kingunge Ngombale Mwiru.

Ni dhahiri basi, kwamba taifa letu limepata pengo, na pengo hili linaweza kuzibwa tu kwa kuendeleza mazuri ambayo tumejitahidi kuyaeleza hapo juu.

Michezo na Mazoezi Katika Islam

Na Latif Mosse

Islamu ni dini inayoendesha maisha ya kila siku ya Mwislamu. Inahusiana na maswala yote ya mtu binafsi na jamii. Kwenye maswala ya mtu binafsi, inahusisha roho, mwili na akili. Islamu inamuhitaji Muislamu awe ni mwenye siha nzuri na nguvu pia, ambayo ni zao la michezo na mazoezi mazuri.

Katika Uislamu, michezo na mazoezi mazuri ni yale yasiyomtoa mtu nje ya muktadha wa kiimani (mikao ya dini). Uislam unaipa michezo na mazoezi umuhimu kiafya, pia kutuwezesha kufanya ibada kama sala, kuhiji Makka na hata kutembea umbali mrefu ili kutafuta sala ya jamaa pamoja na kurahisisha shughuli mbalimbali za kiubinadamu. Ambapo katika hadithi moja iliyosimuliwa na Hadhrat Ibn Umar r.a. ya kwamba mjumbe wa Allah s.a.w Alisema: Kusali pamoja nyuma ya Imamu (jamaa) ni bora mara ishirini na saba kuliko mtu kusali peke yake. (Muslim)

Vilevile, kupitia michezo na mazoezi tunaweza kuimarisha miili yetu na kutuwezesha kufanya shughuli za kimwili. Islam inawahitaji Waislamu wafanye kazi na kuzalisha mali kwa mikono yao wenyewe. Katika hadithi moja inayosimuliwa na Hadhrat Rafii bin Khadij r.a ya kwamba Mtume s.a.w aliulizwa: Ewe mjumbe wa Allah njia gani ya kuchuma riziki iliyo safi zaidi? Akajibu; mtu kufanya kazi kwa mkono wake; na kila biashara iliyo njema (Musnad Ahmad).

Pia kupitia uimara aupatao Mwislamu katika mazoezi na michezo, humuwezesha kufanya majukumu ya kijamii ambayo Mtume s.a.w aliyasisitiza sana hususan kuwatembelea ndugu na wagonjwa. Katika hadithi mojawapo inayopatikana kwenye Tirmidhi, Hadhrat Abu Hurairah r.a. anasimulia ya kwamba mjumbe wa Allah s.a.w alisema aendaye kumjulia hali mgonjwa au kumtembelea nduguye, kwa ajili ya Mungu, Mtangazaji (Malaika) anamtangazia akisema; ufurahi kutembea kwako kubarikiwe na upate makazi katika pepo.

Mtume s.a.w alishiriki katika michezo na mazoezi. Alihitaji Waislamu wawe wenye nguvu na ujasiri katika kukabiliana na maadui wa Uislam pamoja na kuvikabili vitisho dhidi ya dini ya Kiislam.

Mtume s.a.w pia alishiriki kwenye mchezo wa mbio. Imesimuliwa na Hadhrat Aisha r.a ya kwamba yeye alikuwa pamoja na mjumbe wa Allah s.a.w katika safari fulani. Njiani nilishindana nami mbio nami nikampita. Tena baadae siku nyingine ambapo nilikwisha pata kunenepa nikashindana nae mbio. Safari hii mtume s.a.w akanipita na ndipo akasema "Hii ndiyo kulipa safari ile uliyonipita (Abu Daud).

Mtume Mtukufu s.a.w pia alipendelea michezo kama kuogelea, upigaji wa pinde na kupanda farasi. Inasimuliwa katika Sahihi Muslim kuwa Mtume s.a.w alisema "hatua



yeyote bila kumkumbuka Allah ni kupoteza au kutokujali isipokuwa vitendo vinne; kutoka kutembea kwa lengo la kulenga, kujifunza kupanda farasi na kujifunza kuogelea.

Khalifa wa Nne wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) Hadharat Mirza Tahir Ahmad kwa kutambua umuhimu wa michezo na mazoezi kwa Waislam tena bila kujali umri aliandika kitabu kiitwacho Warzish ke zeene" yaani " Hatua za mazoezi" Humo ameandika kuwa, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) aliwahi kukimbia riadha dhidi ya Masingasinga kwa heshima ya Islamu na kuwashinda. Pia anaandika kuwa Hadhrat Musleh Mauood (Khalifatul Masih II) r.a alikuwa anasafiri nje ya Qadian kuwinda na mara mojawapo alishiriki kwenye mbio dhidi ya watoto wake na wafanyakazi wake pembezoni mwa mto Bias. Anaendelea kuandika kuwa Hadhrat Musleh Mauood (Khalifatul Masih II) anasema "Tunafundishwa kuwa na tabia ya kufanya mazoezi ili tuwe wepesi na hai ili viungo vyetu viwe imara ili tuwe majasiri" (Al-Fazl,28March1932 p.2)

Pamoja na faida zote na msisitizo uliowekwa kwenye Islam juu ya kushiriki katika michezo na mazoezi, Tahadhari lazima ichukuliwe kuhakikisha havitusahaulishi lengo letu kuu. Mfano, baadhi ya wanaoshiriki katika michezo husukumwa na utashi binafsi na hupenda kujivuna kwa wengine kwa sababu ya viwiliwili vyao vizuri au misuli iliyojaziwa na wengine husukumwa na mambo mengine mabaya zaidi kuliko hayo. Mwislam lazima aepukane na mambo hayo na ajipambe kwa maadili mema, unyenyekevu na mwenendo wa kujiweka kawaida. Kuchupa mipaka si jambo njema, cha muhimu ni kile cha kukusaidia kudumisha Afya njema, kutekeleza ibada za Kiislam, kushiriki katika jitihada za kumtumikia Allah na kufanya matendo ya ibada kama Hijja yanayo hitaji nguvu za kiwiliwili.

Halikadhalika, Muislamu anapaswa ajiepushe na mazoezi au michezo inayompelekea mtu kupoteza sala, kuacha wazi sehemu za mwili zisizofaa kuachwa wazi, kuchanganyika wake kwa waume, michezo inayohusisha mauwaji au mchezo ya hatari kama mieleka hata wahusika wenyewe hutahadharisha watu wasiige.

Mwisho napenda kuwaasa Waislamu wote wake kwa waume watoto kwa wakubwa kujitahidi kushiriki katika michezo kwani Mtume s.a.w anasema "Muumini mwenye siha (nguvu) ni bora na hupendwa zaidi na Mwenyezi Mungu kuliko muumini dhaifu (Muslim). Kwa rehema za Allah, kwenye Jamati Ahmadiya kuna makundi mbalimbali ya umri na jinsia tofauti (Tanzeem) ambapo wanachama wake wanahimizwa kufanya mazoezi na hushindanishwa mara kwa mara kwenye mikutano yao hususan Ijtimaa. Hii yote ni kuwafanya wawe ni wenye Afya, nguvu na ujasiri kwa ajili ya kuitumikia Islam. Allah Atusaidie tuweze kushiriki katika mazoezi na michezo kwa lengo kuu la kumtumikia Yeye, Inshallah.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Sheikh Abdulrahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Falsafa ya Maombi katika Islam

Kutoka uk. 1

ya ajabu ya kupokelewa kwa maombi yanatokea ambayo yanawastaajabisha watu wasiokuwa Wanajumuiya. Matukio kama haya baadhi yao nitayaweka mbele yenu muda huu.

Mkurugenzi wa idara ya mahubiri Qadian anaandika kuwa Amiri wa wilaya ya Hoshiarpur alimweleza kuwa miaka michache iliyopita katika kijiji chao cha Khera Acharwal kutokana na ukame wa muda mrefu wanakijiji walikuwa na masikitiko makubwa mno hata hivyo maji ya kisima nayo yalikuwa yakikauka na kufikia kiwango cha chini kabisa, wenyeji wengi wa hapa waliokuwa Mabaniani walimwomba Mwalimu wa Jumuiya awaombee. Wao walikuwa na imani kamili ya kuwa endapo watamwomba Mwalimu wa Jumuiya ili awaombee basi lazima mvua itanyesha. Hapo kwanza kabisa Mwalimu wetu aliwafahamisha adabu na njia za kuomba dua na kuwajulisha kuhusu sifa za Mwenyezi Mungu kisha akaongoza maombi. Mwenyezi Mungu Aliyapokea maombi ya Mwalimu huyu wa Jumuiya na kwa Fadhila na Rehema za Allah katika muda wa masaa mawili au matatu mvua ilianza kunyesha. Tukio hilo kwa Fadhila za Allah liliwaachia athari nzuri sana wenyeji wa kijiji hicho na wanakijiji walisema wazi kuwa kwa sababu ya maombi ya Wanajumuiya tu mvua imenyesha.

Hadhrat Khalifatul Masihi atba alisema ya kwamba: "Baadhi ya maeneo kunyesha kwa mvua kunakuwa alama ya msaada wa Mungu na kupokelewa kwake maombi na maeneo mengine kukatika kwa mvua kunakuwa uthibitisho wa kukubaliwa kwake maombi.

Mwalimu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya nchini Guinea Bissau (nchi moja ya Afrika Magharibi) aitwaye Mwalimu Abdallah anasema ya kwamba sisi siku moja tulikwenda kijiji cha Sainchang Kangsa kwa ajili ya kufanya mahubiri na kwa kuwatangazia watu tuliwakusanya na kufikisha ujumbe wa Jumuiya.

Wakati mahubiri yalipokuwa yakifanywa mvua kubwa ilianza kunyesha na kutokana na kelele za mvua kali yeye anasema kuwa sauti yake ilikuwa haiwafikii wasikilizaji na nilianza kujihisi kuwa sasa watu wataanza kutawanyika, yeye anasema ya kwamba wakati ule mimi nilianza kufanya maombi ya kwamba Ewe Mungu mvua hii imetoka Kwako na ujumbe niliokuja nao pia umetoka Kwako lakini kwa sababu ya mvua hii watu hao wameshindwa kuusikiliza ujumbe Wako huu na wapo karibu ya kutawanyika.

Mwalimu anasema, alipomaliza tu maombi haya, Mwenyezi Mungu Akakatisha mvua, yeye anasema kuwa watu mia moja na hamsini waliokuwa wamehudhuria pale wakahubiriwa na kwa Fadhila za Allah baada ya mahubiri kufanyika wote walijaaliwa kujiunga na Jumuiya.

Khalifa Mtukufu a.t.b.a. alisema ya kwamba nikiacha matukio yanayoihusu misimu nayaeleza matukio mengine. Mungu wetu siye Mungu wa misimu peke yake bali ni Mungu Aliye na Uwezo wa kila kitu na Anayasikiliza maombi ya aina zote. Yeye Ana sifa chungu nzima Naye Huonesha udhihirisho wa sifa Zake.

Mwalimu mwingine wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya nchini Benin aitwaye Matini anasema ya kwamba siku chache zilizopita Mwanajumuiya mmoja mpya alikuja kwangu na kusema kuwa mke wangu ana hali tete, Mwalimu anasema ya kwamba mimi nikifuatana na mke wangu nilikwenda nyumbani kwake kwani mke wake alikuwa na shida ya ujauzito na kutokana na homa kali na pia kwa sababu ya kusinyaa kwa mfuko wa uzazi alikuwa ameshindwa kujifungua. Mume wake aliniambia ya kwamba hali kama hiyo imekwishatokea mara mbili kabla ambapo kati ya mama na mtoto angeweza kusalimika mmoja tu hivyo mara zote mbili mama alisalimishwa na mtoto alifariki na sasa hii imetokea mara ya tatu. Mwalimu wa Jumuiya alisema ya kwamba katika hali hii tete sisi pamoja na kutumia dawa pia tufanye maombi. Hivyo anasema ya kwamba mimi nilianza kufanya maombi na baada ya kumaliza maombi na kusoma Sura Fatiha nikapulizia maji na kumnywesha mama huyu, anasema njia hii niliirudia mara mbili mara tatu na kupulizia maji nikampelekea mama huyo.

Mara ya tatu mume wake alitoka nje akiwa na furaha kubwa na kusema kuwa Mwenyezi Mungu Amemsalimisha mke wangu na pia Amenijaalia mtoto wa kiume. Na imani yake huyu mwanajumuiya mpya ilipata kuimarika zaidi juu ya Dhati Tukufu ya Allah na juu ya sifa Yake ya kupokea maombi. Tangu muda ule Mwanajumuiya huyu pia alishika tabia ya kumwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na kwa hamu ya ndani.

Kisha kutoka Karnataka nchini India Amiri wa Wilaya anaandika ya kwamba Rais mmoja wa tawi lake alipata ugonjwa wa uvimbe kwenye ubongo naye akalazwa hospitalini. Madaktari walisema kwamba ugonjwa wake hauwezi kutibika na wakati wa kufanya upasuaji huyu anaweza kupoteza maisha yake.

Yeye mara moja aliniandikia barua ya maombi nami pia nikamtumia jibu lake ya kwamba Mwenyezi Mungu Amponye vizuri. Yeye anasema ya kwamba baada ya mwezi mmoja madaktari walipochukua vipimo vyake kwa mara nyingine basi wakashikwa na mshangao mkubwa mno kwani kulikuwa hakuna hata alama ya ugonjwa ule. Hii ilitokea kwa sababu za Fadhila za Mwenyezi Mungu tu na kutokana na maombi peke yake, Raisi huyu Husein Sahib alipona kabisa.

Latif sahib, Mu'alim katika mkoa wa Morogoro, Tanzania, anaandika: "Kuna mtu aliiba betri za mfumo wa jua katika msikiti wetu. Siku iliyofuata wakati Wanajama'at walipogundua kuhusu hili, waliamua kuwa badala ya kufungua kesi polisi, itakuwa bora kuomba kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Baada ya siku moja tu mtu ambaye alikuwa ameiiba betri ile aliirudisha kwa kuiweka kwa siri mbele ya nyumba ya Sadr wa Jama'at hiyo. "Na anasema kwamba kwa namna hii Allah Mwenyezi alisikia maombi ya Waahmadiya na hili liliwapa nguvu zaidi ya imani katika maombi kwa watu wasio Waahmadiyya ya kuwa Waahmadiya kwa hakika ni watu waadilifu na wakweli.

Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya nchini Guinea Conakry anaandika ya kuwa kijana mmoja Mwanajumuiya mpya alieleza hisia zake ya kwamba anatamani kujitolea maisha yake wakfu na kuitumikia Jumuiya hivyo sisi tulimshauri aende kusoma katika chuo cha Waalimu kilichopo nchini Sierra Leone naye alikubali ushauri wetu na kuanza kujiandaa kwa ajili ya safari yake.

Mbashiri Mkuu anasema kuwa wakati sisi tulipowaita wazazi wake wasiokuwa wanajumuiya msikitini ili tuweze kupata ridhaa yao juu ya hilo basi kidhahiri walifurahi sana na kukusanya taarifa zote na waliahidi kuwa baada ya siku mbili watarudi tena. Baada ya kurudi kwao walimwomba Sheikh wao awape ushauri, Sheikh huyo aliwapotosha na kupeleka mashitaka polisi dhidi yetu ya kwamba Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya si Jumuiya ya Kiislamu na pia ina msimamo mkali na imempotosha kijana huyu na itamfanya kuwa kijana aliye na msimamo mkali.

Mbashiri Mkuu anasema kuwa hapo tulipata wasiwasi sana, naye aliniandikia barua ya maombi nami pia nikamtumia jibu ya kwamba Mwenyezi Mungu Aziteremshe Fadhila Zake, pamoja na juhudi ya hapa na pale pia fanyeni maombi, hivyo anasema ya kwamba wakati polisi ilipofanya uchunguzi na utambulisho wa Jumuiya ulielezwa kwao na wakapewa vipeperushi vya utambulisho wa Jumuiya basi kwa Fadhila za Allah Mkuu wa Polisi alifuta kesi ile na kusema kuwa mimi naona Uislamu uelezwao na hao watu ni Uislamu ulio bora zaidi na wenye amani kuliko Uislamu unaoelezwa na wengine.

Mkuu wa Polisi alisema ya kwamba munipatie maelezo zaidi kuhusu Jumuiya mimi natamani kujiunga na Jumuiya hii.

Mwenyezi Mungu Subhanahu wa Taala kivipi kwa sababu ya kupokelewa kwa maombi ya wanajumuiya Anawajaalia wapate kuimarika katika imani yao na wawe na yakini juu ya Ukhalifa. Kuhusiana na hilo akieleza tukio lake moja mwanajumuiya mmoja wa nchini Mali - Idrees Traore Sahib - anaandika ya kwamba "Mwaka 2008 wakati ilipotimia karne moja ya Ukhalifa nilikuwa nikihudhuria mkutano wa Ukhalifa. Wakati ule mimi nilikuwa nikifanya biashara ya ufugaji wa kuku na nikiacha kuku wote hapo nyuma nikaenda nchini Ghana kwenye mkutano, huku nyuma kuku wote walikufa.

Basi mtu ambaye nilikuwa nimekopa kwake kwa ajili ya biashara hii alipopata kuelewa kuwa mimi ni mwanajumuiya na nilikuwa nimeenda kwenye mkutano wa Jumuiya na hapo nyuma kuku wote wamekufa basi yeye alianza kunipinga vikali zaidi na baada ya kurudi kwangu alinitumia ujumbe kuwa katika muda wa wiki moja tu nirudishie hela yangu iliyokuwa laki moja na elfu hamsini CFA Francs. Yeye anasema ya kwamba mimi nilisikitika mno nikitafakari kuwa fedha sina, sasa mpinzani huyu atanidhalilisha vibaya, usiku kucha niliendelea kufanya maombi ya kwamba Ewe Mungu wangu Unisaidie mimi kutokana na mapenzi ya Khalifa tu nilikuwa nimeenda kushiriki kwenye mkutano, anasema ya kwamba usiku ule niliota ndoto kwamba kuna mazao yamedondoka kwenye lori nami ninayaokota. Yeye anasema, mimi asubuhi mapema nilikwenda sehemu ile ambapo ingawaje sikuliona lori lolote lakini mazao niliyakuta yaliyokuwa yakidondoka kule ambayo nilianza kuyakusanya, basi ghafla niliona kifurushi fulani chenye rangi nyeusi, nilipokifungua kile kifurushi nikazikuta humo hela zipatazo laki moja na elfu hamsini CFA Francs. Mimi niliwauliza baadhi ya watu wa maeneo yale basi waliniambia ya kwamba usiku wa kuamkia leo lori moja lilikuwa limesimama hapa ambalo sasa lilikuwa likienda Senegali. Mimi niliwaambia kuwa kuna pesa ambayo nimeikuta hapa ikiwa kuna mmiliki wake basi aniambie na kuchukua hela yake lakini hakuna mtu yeyote aliyejitokeza akidai kuwa hii ni pesa yake.

Kwa vyovyote mtu aliyekuwa ananidai alipokuja kwangu na kuniomba nilipe deni langu nikasema subiri kidogo nalipa mkopo huu, Mwenyezi Mungu Amenisaidia na nikamrudishia hela yake yote. Sasa anasema kuwa miaka mingi imepita juu ya tukio hilo na mpaka leo hakuna mtu yeyote aliyedai kwamba ile pesa ilikuwa pesa yake.

Hadhrat Masihi Mauud a.s anasema ya kwamba katika kanuni ya Mwenyezi Mungu ipo mifano ya kukubaliwa kwa maombi na kutokana na kanuni hiyo hiyo katika kila zama Mwenyezi Mungu Huteremsha mifano iliyo hai na endapo tunatamani kupata sehemu katika mifano ya kukubaliwa kwa maombi basi yapo baadhi ya masharti na vipengele ambavyo hatuna budi kuyatekeleza.

Katika masharti ya maombi jambo la kwanza kabisa linalotakiwa lizingatiwe ni kutenda matendo mema na kuwa na imani thabiti. Mtu asiyerekebisha itikadi zake na kutenda matendo mema wala hayaboreshi matendo yake na anafanya maombi, mtu huyo ni kana kwamba anamjaribu Mwenyezi Mungu.

Basi kuna haja ya kurekebisha hali ya imani na matendo vile vile. Haiwezekani ya kwamba sisi katika nyakati tano za sala tusizingatie sala wala tusitimize haki za msingi za binadamu na ikitokea shida yoyote basi wakati ule tuanze kumkumbuka Mungu pia tukumbuke wajibu wetu wa kutimiza haki za binadamu, hivyo kwanza kabisa tutalazimika kujirekebisha. Hali ya kuwa na itikadi sahihi tu haiwezi kutusaidia mpaka tuwe tunatenda matendo mema.

Na matendo mema ndiyo haya tu ya kwamba haki za Mwenyezi Mungu pia zitimizwe na haki za viumbe vyake vile vile zitimizwe, ikiwa tutatekeleza hayo basi Mwenyezi Mungu pia Atapokea maombi yetu.

Mwenyezi Mungu Atujaalie kuyabadilisha maisha yetu sawa na amri Zake na muda wote Atujaalie tuweze kuzitimiza haki za maombi na ibada Zake. Aamin.

Ufafanuzi: Mimi ni Mwisho wa Manabii na Msikiti wangu ni Mwisho wa Misikiti

Kutoka Maktaba Zetu

Inasemwa kwamba Hadithi fulani za Mtukufu Mtume s.a.w. zinapinga itikadi ya kuendelea Unabii.

Mathalan alisema: "Mimi ni mwisho wa Manabii," na tena "hapana Nabii baada yangu."

Inafuata ya kwamba kwa hadithi hizi, hakuwezi kuwa Nabii wa namna yoyote baada ya Mtukufu Mtume s.a.w.!

Inasikitisha ya kwamba hao wanaotaja Hadithi hizi za Mtukufu Mtume s.a.w., wanasahau ya kuwa maneno "Mimi ni mwisho wa Manabii" yanafuatwa na maneno ya maana sana "na msikiti wangu ni mwisho wa misikiti" (Muslim jalada la kwanza).

Kwa hiyo kama Mtukufu Mtume ni mwisho wa Manabii hasa, basi msikiti alioujenga Madina ni mwisho wa misikiti hasa. Itakuwa kosa kujenga msikiti wowote baada ya msikiti wa Mtukufu Mtume s.a.w. wa Madina.

Lakini hakuna anayeona upinzani katika maana iliyowekwa juu ya sehemu ya kwanza ya Hadithi hii na maana iliyowekwa juu ya sehemu ya pili ya Hadithi hii hii.

Sehemu ya kwanza inasemwa ina maana ya kukomesha unabii wa kila aina baada ya kufika Mtume s.a.w.

Lakini sehemu ya pili haisemwi kama hivi kuwa na maana ya kukomesha ujenzi wa misikiti. Watu haohao wanaosadiki kukoma kwa Unabii, hawaoni ubaya wowote kwa kujenga misikiti zaidi. Kwa kweli ari yao ya kujenga misikiti imepita kiasi.

Kuna miji yenye misikiti zaidi kuliko inayohitajiwa hasa; hivyo mingi inabaki mitupu. Katika miji mingi misikiti inapatikana hatua chache mmoja baada ya mwingine, hivi kwamba wingi wao uko dhahiri.

Kama maneno "mwisho wa manabii" yanaleta maana ya kukomeshwa kwa Unabii, basi maneno, "Mwisho wa misikiti" ni lazima yalete maana ya kukomeshwa kujengwa kwa misikiti baada ya msikiti wa Mtukufu Mtume s.a.w. Ili kuwa na hakika, kunajaribiwa kutafutwa vitatuzi vya taabu hii.

Inasemwa ya kuwa misikiti inayojengwa na Waislamu baada ya wakati wa Mtukufu Mtume s.a.w. ni misikiti inayojitolea kwa ajili ya ibada iliyofundishwa na Mtume s.a.w. Inajengwa kwa makusudio yaleyale ambayo kwayo Mtukufu Mtume s.a.w. alijenga msikiti wa kwanza.

Kwa hiyo, misikiti inayojengwa na Waislamu ni misikiti ya Mtukufu Mtume s.a.w. mwenyewe.

Haiwezi kutengwa mbali na mfano inayouiga. Misikiti haiwezi na haipingi umwisho wa msikiti wa Mtukufu Mtume s.a.w. Tatuzi hili ni la kufaa sana.

Lakini vilevile inafaa kusema kwamba maneno "Nabii wa mwisho" hayakatazi kufika kwa Manabii wanaoiga maisha ya mfano wa mtukufu Mtume s.a.w., ambao hawafundishi chochote kipya, ambao wanamfuata yeye tu na mafundisho yake; ambao wanapewa kazi ya kueneza mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w., ambao wananasibisha neema za kiroho walizopata pamoja na unabii kwa mfano wa kiroho wa mvuto wa mwalimu wao na bwana wao, Mtukufu Mtume s.a.w. Kuja kwa Manabii hawa hakuendi kinyume dhidi ya haki ya Mtukufu Mtume s.a.w. kuwa "nabii wa mwisho"; kwa njia ileile na kwa sababu ileile ambayo kwayo kujengwa kwa misikiti leo hakuendi dhidi ya daraja ya msikiti wa Mtume s.a.w. kuwa "Msikiti wa Mwisho".

Sasa, hebu tuirudie Hadithi ile isemayo "hapana Nabii baada yangu." Hadithi hii haiwezi kuwa na maana hasa kwamba hakuwezi kuwa Nabii baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. Hadithi hii vilevile ina maana hii tu:

Kwamba hakuna Nabii anayeweza kuja sasa ambaye atatengua mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. Hadithi hii ya Mtume s.a.w. inaelekea kwenye neno baada. Jambo fulani linakuja baada ya jingine hapo tu jambo la kwanza linapokwisha na la pili linashika mahala pake. Nabii anayefika kwa ajili ya kutangaza, na kwa kila njia, kusaidia na kukuza unabii wa Mtukufu Mtume s.a.w., hawezi kusemwa amefika baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. Unabii wa Mtukufu Mtume s.a.w. utakuwa palepale.

Nabii anayekuja kuutumikia Unabii huu ni sehemu ya silsila ya Mtukufu Mtume s.a.w. Nabii angeweza kusemwa amefika baada ya Mtukufu Mtume s.a.w., kama angeleta kutenguliwa kwa sehemu yoyote ya mafundisho ya Mtukufu Mtume s.a.w. Mtu mwenye busara hujaribu kufikiria kwa makini kila madhumuni yenye maana na kupata undani wa maana ya hilo kila neno lililomo ndani yake.

Si la ajabu, Bibi Aisha r.a., mke wa Mtukufu Mtume s.a.w., akihofia Waislamu watakaofika baadaye wasije wakaikosa maana ya Hadithi ya Mtukufu Mtume s.a.w. juu ya Unabii aliwaonya watu akisema:

"Semeni yeye (Mtume s.a.w) ni Khaatamannabiyyin wala msiseme hakuna Nabii baada yake" (Takmila Majma'-ul-Bihaar, uk. 85).

Kama katika maoni ya Bibi Aisha, kama katika ujuzi wake, kuja kwa Manabii kulikwisha hasa kwa nini aliwaonya watu dhidi ya kusema kuwa hakuna Nabii baada ya Mtukufu Mtume s.a.w.?

Kama alipotoa onyo hili, alikosea, na aliyosema yalikuwa kinyume cha mafundisho ya Mtukufu s.a.w., kwa nini Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. hawakumpinga?

Onyo lake dhidi ya Hadithi "hapana Nabii baada yangu" linaonesha waziwazi ya kuwa kwa maoni yake, kuja kwa Nabii baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. kunawezekana.

Ila tu, Nabii kama huyo hawezi kuwa mletaji wa sheria, au Nabii asiyemtegemea Mtukufu Mtume s.a.w. Kule kupokea kwa Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. onyo hili la bibi Aisha bila ya hoja au kupinga, kunaonesha kwamba Masahaba wa Mtukufu Mtume s.a.w. walifahamu aliyoyasema na kuamini aliyoamini.

Ukweli Kuhusu Ibilisi na Sheitwani

Kutoka uk. 1

kwani kwa mujibu wa Qur`an Tukufu ni kwamba Ibilisi naye aliamrishwa kumtii Adam, kwani Allah Alisema'' Nini kilichokuzuia kutii nilipo kuamuru? (7:13). Maneno haya yanaonesha kwamba Ibilisi ingawa si Malaika lakini pia aliamrishwa kumtii Adam. Pia Malaika hapa wanaweza kuwa kama wawakilishi kwa ajili ya viumbe wengine pia, kwa kuwa kwao wawakilishi wa Sifa za Mungu basi Amri inayotolewa kwao huwahusu viumbe wengine pia. Ni kama vile amri zote za Qura`an Tukufu zinazowahusu Waaminio kama vile, kusali, kufunga, kuhiji, n.k Ingawa kama amri zimeelekezwa kwa waaminio tu lakini haina maana kwamba makafiri hawatahukumiwa kwa kuacha sala. Ibilisi sawa na maana za neno lenyewe katika lugha ya Kiarabu yawezekana kuwa ni jina la sifa linaloihusu nafsi ya uovu iliyo kinyume na Malaika. Huyo aliitwa Ibilisi kutokana na kuwa na sifa nyingi zilizotajwa katika maana ya neno lenyewe. Ukweli ni kwamba Ibilisi siye yule shetani aliyetajwa kwenye (2:37) aya inayofuatia ile imhusuyo Ibilisi. Ingawa majina Ibilisi na shetan yametumika pamoja hata kwamba mtu angeweza kudhani kuwa yamemhusu mtu mmoja. Lakini kama isomwe kwa makini Qur`an Tukufu inatoa tofauti ya wazi kuhusu matumizi ya majina hayo mawili ingawa yote yanamuashiria mtu muovu. Tofauti inayoeleweka sana ya majina haya ni kwamba kila mara Qur`an Tukufu inapomzungumzia yule muovu aliyekataa kutii pamoja na Malaika hutumia jina la Ibilisi, lakini kila inapomzungumzia yule muovu aliyeingia Bustanini na kumpoteza Adam jina la sheitan hutumika. Na jambo hili limetumika mara zote ndani ya Qur`an Tukufu iliposimulia kisa cha Adamu. Tazama Qur`an Tukufu juu ya kisa hiki (2:35,37 7:12,21, 15:32, 17:62, 18:51; 20:117,121; 38:75). Hzi zinathibitisha kwamba ibilisi yule aliyetofautiana na Malaika katika utii siye yule shetani aliyesemezana na Adamu bustanini ambaye alikuwa miongoni mwa watu ambao Adam alitumwa kwao kama Nabii na mrekebishaji mkuu wa jamii. Kwa hivi ibilisi hakuwa Malaika hii ni wazi kutokana na ukweli kwamba sifa za viumbe hao wawili hutofautiana sana. Wakati Malaika husema kuwa daima ni wenye kumtii mola wao (Qur`an 16:51) Ibilisi anaonyeshwa ndani ya Qur`an Tukufu daima ni mwenye kuvunja amri za mola wake. (7:12-13). Pia mahala pengine katika Qur`an Tukufu Ibilisi anasemwa kuwa anatokana na majini (18:51) Aya hii bila shaka inabainisha utofauti wa viumbe hao hata kikhulka. Pale ambapo Ibilisi kimaumbile anahusishwa na majini ambao Qur`an Tukufu inasema waliumbwa kwa moto (55:16) Malaika inasimuliwa kuwa waliumbwa kwa nuru. Hapa yafaa jambo moja lieleweke kwamba Ibilisi na Shetani ndio wanaopatana zaidi kwa sifa na wala si Malaika. Ukisoma maelezo yanayotolewa na Qur`an Tukufu kuhusu viumbe hawa utagundua mfanano mkubwa ingawa Sheitani lina upana zaidi. Kama ilivyo kwa Ibilisi ambaye ni mwasi hali kadhalika Sheitani na hawa wote wawili wame laaniwa na Mungu. Wote wawili ni wapotevu na wapotezaji wa viumbe wengine (4:120-122, 2:35) Kwa hivi ibilisi na sheitani ndio wanaoelekea kuwa washirika wakubwa wanao fanana kihulka. Neno limetumika katika Qur`an Tukufu kuonyesha ile roho ya kiburi na chanzo cha uasi. Ilhali neno shaitani linairejea ile dhati iliyopotea na yenye nguvu ya ushawishi juu ya mwingine kwa hivi hata ibilisi ana sifa ya ushetani kwa maneno mengine vitu vyote vibaya, vichafu na vinavyozuru huitwa sheitani katika lugha ya Kiarabu, hata waovu ni mashaitani wapinga ukweli ni sheitani, wanyama hatari ni sheitani, magonjwa sugu ni shetani na hata bakteria na virusi wabaya wameitwa mashaitani. Kur`an Tukufu, hadithi na vitabu vya lugha ya Kiarabu vimejaa mifano mingi ya matumizi hayo niliyoyataja. Tunaona kuwa Qur`an Tukufu imewaita mashetani hata wanafiki na wafanyao uasi katika nchi (2:15). Mtume mtukufu s.a.w alimuita sheitani hata yule mwizi aliyemkaba Abu Hurairah r.a mara kadhaa (Bukhari). Pia mbwa mmoja mweusi wa mtaani (mbwa koko) aliitwa sheitan na Mtume s.a.w . (Sunan Ibn Majah). Mtume s.a.w aliwashauri masahaba zake kufunika vyombo vyenye vyakula na vinywaji ili sheitani asiingie humo (Ibn Majah). Hapa ni dhahiri alimaanisha vijidudu vya magonjwa. Katika kitabu cha Muslim kuna hadithi ambapo Mtume s.a.w anawashauri waaminio kusafisha pua zao mara tu waamkapo kwa sheitan hurandaranda humo usiku kucha. Hivi sasa imefahamika kisayansi kwamba bakteria na vumbi lenye sumu haviingii puani wakati wa usingizi na hivyo ni vyema kusafisha asubuhi. Kwa hivi kutokana na mifano hiyo hapo juu ni wazi kwamba shetani ni neno la jumla lililo pana mno kimaana ambalo huweza kutumiwa juu ya vitu na watu mbalimbali. Ilihali ibilisi ni neno lenye maana moja ya msingi ukataaji na kiburi ambalo Aghalabu huwa wapingaji na makafiri waliozikatia tamaa Rehma za Allah.

Sheikh Abdul Qadir: Kutoka Ubaniani Hadi Uislamu

Na Sheikh Muzaffar Ahmad Durran - Pakistan

Sheikh Abdul Qadir alizaliwa tarehe 15 Agosti 1909 katika nyumba ya Mbaniani Khatri huko Gorana Pathanan, Kata ya Bhalwal, wilaya ya Sargodha, India. Wazazi walimpa jina Sodagar Mal. Baba yake Lala Wazir Chand aliwezaje kujua kwamba mtoto wake anayeitwa Sodagar Mal kulingana na biashara yake, katika zama zijazo atakuwa mwana biashara wa kiroho kwa kutumikia Islam na siku itawadia atakapoongoza wengi.

Sodagar Mal alipata masomo ya awali katika kijiji chake. Alihitimu masomo yake ya kati katika shule ya kati ya Lalian, Wilaya Sargodha. Masomo ya mbele bado yalikuwa katika mazungumzo, katika hali hiyo alihamia kwa familia yake Dhakhira Beranwala, kata ya Hafidh Abad, wilaya ya Gujaranwala kutoka wilaya ya Sargodha, alisaidia katika biashara ya familia, katika hali hiyo Mungu Alimfungulia mlango wa Islam. Ilitokea hivi kwamba katika kijiji kile kile cha kata ya Hafidh Abad ambapo alikuwepo Sodagar Mal, kijana mzuri Mbaniani, humo humo alikuwepo mwenye duka Mian Muhammad Murad, Mwislamu Mwaahmadiyya aliyetambulika kwa uzuri na ukweli wake mpaka mbali.

Sodagar Mal na sasa Sheikh Abdul Qadir alijuana na Mian Muhammad Murad. Yeye akiona alama ya mwongozo na uzuri katika kijana huyo alianza kumhubiri. Hapo mafundisho sahihi ya Islamu yalianza kuathiri moyoni.

Mian Muhammad Murad wakati wa kuenda Mkutanoni wa Mwaka wa 1924 alimchukua mwenyeji mmoja Bwana Allah Jawaya Msali, aliyerudi kwa athari nzuri sana kwa kuzuru Qadian na kuona mazingira ya pale. Lakini alipoulizwa na watu alianza kusema kwamba katika Qadian kuna biashara na udanganyifu tu. Kwa Sodagar Mal hali hiyo ilikuwa swali kubwa. Aliona kwamba mkazi wa Qadian Mian Muhammad Murad anaishi maisha safi na matakatifu na watu wanasifu hulka zake lakini Allah Jawaya Msali anasema kwamba katika Qadian kuna biashara na udanganyifu tu. Kusuluhisha tatizo hilo Bwana Sodagar Mal aliona muhimu kumwona Allah Jawaya peke yake. Basi Alimwita Allah Jawaya kwenye duka la ndugu zake wakikaa juu ya rundo la pamba alimwuliza kwamba unasema kwamba katika Qadian kuna biashara na udanganyifu tu lakini huyo Muhammad Murad ni mbali sana na hali hiyo na anaishi maisha mazuri, kuna nini hapa?

Mara Allah Jawaya alisema kwamba kauli yangu ni uongo, mimi ni maskini wa kijiji, matajiri wa kijiji wanawapinga Waqadiani, kwa hiyo siwezi kusema kweli mbele ya watu. Nawaambia watu wa kawaida sawa na ridhaa yao ili wafurahi waila ukweli ni huu kwamba kama Islam inapatikana popote duniani basi ni katika Qadian tu. Nakuambia jambo hili la kweli, kama nikiwaambia watu wengine jambo hilo hilo, matajiri wa kijiji watanifukuza kutoka kijijini



Sheikh Muzaffar Ahmad Durran - Pakistan

wakinipiga kwa viatu. Kwa hiyo mbele yao nitasema jambo lile lile. Lakini ukweli ni huu niliyokuambia. Kwa maongezi haya ya Allah Jawaya sio tatizo la Sodagar Mal liliondoka bali aliinuka humo kwa azma hii kwamba mimi mwenyewe nitaenda Qadian na nitashuhudia hali kwa macho yangu tu. Ingawa Sodagar Mal alichukia Islam kwa kuona hali duni, kutokuwa na elimu, kukosa hulka na hali mbaya ya kiuchumi ya Waislamu wa kawaida. Lakini mambo halisi ya kuvutia ya Mian Muhammad Murad na mfano wake mwema wa kushinda moyo alimlazimu kwamba akienda Qadian ashuhudie hali ilivyo mwenyewe. Wakati ule alibanwa na hali. Kwa ulimi alisema kwamba hata kama dunia yote isilimu sitasilimu lakini moyo ulivutika sana humo kwa nguvu.

Baada ya maongezi ya juu kwa Allah Jawaya kesho yake asubuhi tu Sadagar Mal akawa tayari kwenda Qadian. Alimwambia Mian Muhammad Murad kwamba ninaenda Qadian. Mian Muhammad Murad alisema kwamba maongezi yako ya jana usiku kwa Allah Jawaya niliyasikiliza kwa masikio yangu katika giza la usiku. Wakati ule ule nilinuia moyoni kwamba kama Sodagar Mal akawa tayari kuenda Qadian basi tutaenda pamoja. Kwa hiyo naenda nawe.

Basi baada muda mfupi tu wote wawili waliondoka kwa kuelekea Qadian. Wakitoka Sangla Hill badala ya Batala walishuka Stesheni ya China, stesheni mbele ya Batala, ili jamaa wa Sodagar Mal wakiwafuata isije wawakamate njia ya miguu kati ya Batala na Qadian. Msafara huo kutoka China ulifika Qadian. Sodagar Mal mara baada ya kufika Qadian alieleza katika nyumba ya wageni kwamba miye Mbaniani, kwa hiyo sitakula chakula kilichopikwa na Mwislamu yeyote. Siku zile mwalimu wetu Hadhrat Mir Muhammad Is'hak alikuwa msimamizi wa nyumba ya wageni na alipewa uwezo maalumu kutoka kwa Mungu ya kutumikia wageni. Basi alipanga kuagiza chakula cha Sodagar Mal kutoka nyumba ya Mabaniani na mpango huo uliendelea kwa wiki moja mfululizo. Katika muda huo Mian Muhammad Murad alimkutanisha Sadagar Mal na wazee wa Kiahmadiyya wapya waliosilimu kutoka Mabaniani na Masingasinga. Kukutana na ndugu Hadhrat Abdur Rahim ra, ndugu Hadhrat Abdur Rahman Qadiani, Hadhrat Masta Sardar Abdur Rahman B.A. ra Hadhrat Sheikh Ghulam Ahmad Waidh ra na Hadhrat Sheikh Muhammad Yusuf ra, Mhariri wa gazeti Nur Qadian kuliatharisha sana moyo wa Sadagar Mal, kwani watu hao walitokana na Masingasinga na Mabaniani. Na kwa kusilimu walipata nuru maalumu na maisha ya kiroho. Mian Muhammad Murad alimkutanisha na wazee Waislamu wa zamani pia ambao walipata Baraka maalumu za Jumuiya Ahmadiyya. Maongezi yaliyojaa na ikhlasi na mifano bora ya Hadhrat Maulawii Rajiki ra, Mualimu wangu Hadhrat Hafidh Roshan Ali ra, Hadhrat Khalifa Rashiduddin ra, Hadhrat Maulawii Dhulfikar Ali Khan ra na Hadhrat Maulawii Abdul Mughni ra ililazimu moyo wa Sodagar Mal kuwa Sheikh Abdul Qadir.

Bado ikawa wiki moja tu tangu Sodagar Mal aje Qadian, kikundi cha watu saba cha jamaa zake kikaja Qadian kwa kumrudisha. Watu hao walimwona Hadhrat Chaudhari Nasrullah Khan, siku zile aliyekuwa Nadhir Aalaa kiheshima na walisisitiza kwamba Sodagar Mal arudishwe nao. Bwana Chaudhari alisema kwamba ni mafundisho ya Islam: لا إِكۡرَاهَ فِى ٱلدِّينِ kwamba hakuna karaha katika dini wala hiyo haijuzu. Kama Sodagar Mal akitaka kuenda nanyi basi bila shaka mchukueni.

Jamaa walimwambia Sodagar Mal kuenda nao kwao lakini yeye ameshakuwa Abdul Qadir moyoni. Kwa hiyo alikataa kuenda nao na alianza kuishi katika makao ya kutangaza Islam katika hali yoyote.

Siku ya pili au tatu Sodagar Mal alimwomba Khalifatul Masihi II akikubali baiti yake amwingize katika Jumuiya Ahmadiyya. Hapo Hudhur ra alisema kwamba kuna haraka gani. Subiri miezi 2-3 zaidi lakini aliomba kwa msisitizo kwamba Hudhur, nimeshapata yakini juu ya ukweli wa Islam. Hapo Hudhur ra alimwambia mwalimu wangu Hadhrat maulana Seyyid Muhammad Sarwar Shah ra kwamba msomeshe shahada leo leo, kesho tutapokea baiati. Basi ikafanyika hivyo, sasa Lala Sodagar Mal akawa Sheikh Abdul Kadir. Alhamdulillah, thumma Alhamdulillah.

Ilikuwa athari kubwa ya tamaduni ya kibaniani kiasi hiki kwamba juu ya kusilimu mwanzoni mwanzoni Bwana Sheikh alikuwa akila chakula kwa shida sana kilichopikwa na Mwislamu. Lakini baada ya siku chache aliungana kiasi hiki kwamba ikawa ngumu kutambua kwamba kijana huyu amesilimu kutoka kwa mabaniani au ni Mwislamu wa kuzaliwa. Kwa kweli mabadiliko hayo kikamilifu yalikuwa matokea ya lazima ya ikhlasi ile aliyokuwa na Sodagar Mal moyoni mwake kwa dini. Islam ilinurisha sana ikhlasi hiyo.

Ilipopita miezi michache tu tangu Sheikh Abdul Qadir alipata kuzaliwa kiroho, Pandat Mashuhuri wa Sanatan Dharm Bwana Raj Narain Arman akaja Qadian. Sheikh Abdul Qadir alishajiunga na Madrasa Ahmadiyya. Mabaniani wachache wa Qadian walimleta Pandat Raj Narain kwa kumtembeza Madrasa Ahmadiyya. Kwani Kutoka Madrasa Ahmadiyya tu wabashiri vijana walikuwa wanatoka ambao walishindana na Aariya Samaj na Ukristo kwa ujasiri sana. Kwa bahati tu wakati ule Sheikh Abdul Qadir, Mwislamu Mpya alisimama uani na Mabaniani wa Qadian walishajua kusilimu kwake. Mbaniani mmoja akimwashiria Bwana Sheikh alimwambia Bwana Pandit Kwamba kijana huyu pia alikuwa mbaniani lakini sasa ameshasilimu. Bwana Pandit alimwendea Sheikh Abdul Qadir moja kwa moja na kamwuliza kwamba Islamu ina uzuri gani ambao unakosekana katika dini ya Kibaniani. Baada ya kutafakari kidogo kijana Abdul Qadir alimwuliza Bwana Pandit kwamba uniambie kwamba lengo la dini ni nini? Bwana Pandit alijibu kwamba kukutana na Mungu. Hapo Abdul Qadir alisema kwamba umeshapata kukutana na Mungu? Bwana Pandit alijibu kwamba hapana. Hapo Bwana Sheikh alimwuliza kwamba sawa na elimu yako je, kuna Mbaniani mmoja aliyekutana na Mungu? Sasa pia Bwana Pandit alikanusha lakini pia alisema kwamba naweza kusema kuhusu Bwana Ram Chandar na Bwana Karishna. Sheikh Abdul Qadir alisema kwamba nataka kumwona Mbaniani yeyote wa namna hii katika zama hizi. Hapo Bwana Pandit alimwuliza kijana Mwislamu Mpya kwamba je, waweza kutaja jina la Mwislamu yeyote ambaye amepata kukutana na Mungu? Bwana Sheikh mara alitaja jina la Hadhrat Masihi Mau'udi as na alieleza kama ukweli wake ufunuo:

ياتون من كل فج عميق

yaani watu watamfikia kutoka sehemu mbali mbali. Hapo Mabaniani waliokuwa pamoja walimwita Bwana Pandit na walienda upande mwingine.

Maongezi hayo ya kawaida ambayo Sheikh Abdul Qadir aliyofanya katika siku zake za awali na mjadili mkubwa wa Kibaniani yanaonyesha wazi wazi jambo hili kwamba Bwana Sheikh alikuwa makini kwa itikadi yake na kijana mwekaje lengo lake mbele yake.

Sasa Bwana Sheikh alikuwa miongoni mwa wanafunzi wazuri wa Madrasa Ahmadiyya, mwanafunzi mwenye kuheshimu na juhudi. Katika 1931 alipata shahada ya usheikh katika mtihani wa chuo cha Panjab (Panjab University). Baada ya kupata mazoezi ya mahubiri kwa muda fulani katika 1934 alianza kazi ya mahubiri.

Bwana Sheikh alikuwa akitoa hotuba yenye athari lakini alikuwa akiepa tu kutoa hotuba iwezekanavyo sawa na tabia yake. Alikuwa akiongea kwa jadhba na sauti ya athari katika mjadala. Alikuwa akimkamata vizuri mpinzani.

Baada ya uhuru wa Pakistan, 1947 alihamia pale na aliendelea kutumukia dini ya Allah.

Bustani ya Washairi

CHE MOSSE KATANGULIA (1950 – 2017)

Na Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

419. Kiongozi wa busara
Aliyejaa sitara
Mpole hana harara
Mambo kuyapapukia.

420. Anasema kwa kupima
Kila neno la hekima
Yu mbali na uhasama
Na mambo ya kuchochea.

421. Selemani wa Madishi
Ni fundi wetu aushi
Alikuwa kwenye jeshi
Lilokwenda kukagua.

422. Kwa kazi za Jumuia
Apenda kujitolea
Kipaji akitumia
Kuyaleta manufaa

423. Ilikuwa ni sururi
Kuona sehemu nzuri
Tukarudi kwa Amiri
Habari kumpatia.

424. Kazipata kwa furaha
Sote tulihisi raha
Mwisho katupa nasaha
Sehemu kuongezea

425. Sehemu zote jirani
Zile ziko mpakani
Watufanyie hisani
Waweze kutuuzia.

426. Ongezeni ongezeni
Hatujui ya mwakani
Aridhi ina thamani
Bei wataongezea.

427. Na hata wanajamati
Wasiwe nyuma katiti
Aridhi wapate hati
Aridhi kujipatia.

428. Katu sifanye ajizi
Aridhi kitu azizi
Bila aridhi huwezi
Huwezi kuendelea.

429. Kazi hii adhimu
Alipewa muadhamu
Ngumbewe Mukaramu
Apite akinunua.

430. Kaifanya kwa makini
Abudu wa Rahmani
Ulimi wake laini
Na uzuri wa tabia.

431. Hakuwa nayo papara
Taratibu kwa ishara
Aliepusha madhara
Mwana diplomasia.

432. Sehemu nyingi hakika
Ikawa kubwa baraka
Tukaweza kuzishika
Kuwa mali ya jamia.

433. Hapo ikaanza kazi
Tukaikata minazi
Mahali pawe ni wazi
Tupate pa kuanzia.

434. Akaanzisha kamati
Isimame iwe kati
Ujenzi ijidhatiti
Shule kuisimamia.

435. Wajumbe akateua
Wawe wa kusimamia
Shule ya Ahmadia
Kitonga namalizia.

436. Wajumbe nakutajia
Amiri kawateua
Ujenzi kusimamia
Hadi mwisho kufikia.

437. Mwenyekiti ni Wamamba
Mahadhi mvuta kamba
Katibu kashika namba
Nyuma hakuangalia.

438. Sheikh wetu bini Ame
Alisimama kiume
Haraka kama umeme
Kazi kuzifatilia.

439. Mweka fedha Mgeleka
Musa hakupumzika
Kila kona kazunguka
Mradi sije sinzia.

440. Bingwa muhamasishaji
Mzaliwa wa Ujiji
Juma ni mpiganaji
Msalizi hakutulia.

441. Pazi mwana wa Kitabu
Alitimiza wajibu
Kazi akaziratibu
Hata kwa jasho kutoa.

442. Hamisi mwana wa Mbanga
Kasaidia kupanga
Ni vipi tutaijenga
Shule ya Ahmadia.

443. Bwana Yusufu Malinda
Mtihani alishinda
Wa kutoa bila inda
Amiri Kumteua

444. Timu ilifanya kazi
Kwa mapenzi na uwazi
Walosema hatuwezi
Wakabaki kushangaa.

445. Ni kamati ya ujenzi
Tena ya wakurugenzi
Wakafanya kwa mapenzi
Bukratan wa aswia

446. Michango walitafuta
Huko subira wavuta
Kazi kubwa ilipita
Ili watu kuchangia.

447. Ni asubuhi, jioni
Hodihodi majumbani
Hata huko Ofisini
Michango kukumbushia.

448. Hatukuwa na hasira
Ila wingi wa busara
Tukashika kwa imara
Nguzo kuzingatia.

449. Kwenye sala tuliomba
Kwa Mola wetu Muumba
Tusijepata kuyumba
Na kazi tukalegea.

450. Dua zilikubaliwa
Mipango yetu ikawa
Ikaenda sawa sawa
Vikwazo vikapungua

451. Mola katupa wepesi
Nao wingi wa nemsi
Tukajenga bila wasi
Mashaka kuyaondoa.

452. Milango ikawa wazi
Ukaisha utelezi
Kwa siku hadi miezi
Kazi ikaendelea.

453. Vikwazo vikaondoka
Kwa baraka za Rabuka
Palo pinda kunyooka
Rabbi katuzidishia.

454. Na Khalifa Mtukufu
Katupatia balafu
Fungu lililo nadhifu
Tukapata endelea.

455. Hicho kipindi kigumu
Amiri wetu adhimu
Yeye kwetu alidumu
Sisi kutusaidia.

456. Mawazo na ndarahima
Alitupa na mapema
Na sisi imma fa imma
Mbeleni tukasogea.

457. Alituunga mkono
Kwa vitendo na maneno
Na penye msuguwano
Utata aliutoa.

458. Aliibeba moyoni
Kuiweka akilini
Shule aliithamini
Kwake ilitangulia.

459. Kazi tukakamilisha
Fanikio la maisha
Nyoyo tukazidhamisha
Kumshukuru Jalia.

460. Ashukuruwe Kahari
Shule yetu yanawiri
Wanafunzi wana ari
Waweza kuendelea.

461. Ni kumbukumbu adhimu
Kumbukumbu ya kudumu
Ya kuipenda elimu
Mosse ametuachia.

462. Sisi ni wako Manani
Na kwako ndio nyumbani
Mauti kwetu yamini
Lazima yatatokea.

463. Mikono tunainua
Tunakuomba Jalia
Twaomba kumpokea
Pepo kumfungulia.

464. Popote pa upungufu
Yailahi ya Latwifu
Mfanyie taklifu
Makosa kumfutia.

465. Kaditamati watama
Utenzi hapa ni tama
Tunakuomba Karima
Mjao kumpokea.

=== Mwisho ===

KHUDDAMUL AHMADIYYA.

SEHEMU YA PILI:
Kutoka toleo lililopita:-

26. Hatusikii kwa nini, wasuni kung'ang'ania
Tueleze kwa undani, maana umepania
Unajivunia nini, Kushindana na dunia?
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

27. Tembeleeni kusini, Nachingwea ulizia
Kama watoka sokoni, kwa upande wa kulia
Msing'ang'ane Mjini, Lajna kugombania
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

28. Lo! inatuhusu nini!, Kijana nakuambia
Hausikii kwa nini?, ndoa twaisubiria
Achana na upagani, utakuja kujutia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

29. Hapa hapa duniani, ndipo pakujifunzia
Tuwaoe wa kundini, tupate kujazilia
Msisahau Manyoni, wengine wamebakia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

30. Ukikamatwa ugoni, utakuja tulilia
Tueleze kwa undani, acha kusikilizia
Chukua uweke ndani, ndoa tamu nakwambia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

31. Uzuri wa humu ndani, tunajuana tabia
Sio kidogo nje ndani, huko usitie nia
Tuwaoe wa kundini, mimi nawahurumia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

32. Mapenzi yetu kwa wote, na chuki si kwa yeyote
Ninawaombeni nyote, msiipoteze kete
Pia tuungane sote, kuoana kivyovyote
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

33. Mzee Duage yumo, vifaa vimebakia
Yaliyomo pia yamo, kijana changamkia
Oa uwe na mfumo, tupanue Jumuia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

34. Msituchague sana, wadada tafadhalini
Ili msipate lana, muoleweni kundini
Ndoa jambo la maana, achaneni na wasuni
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

35. Jama tuhurumieni, mpunguzeni vigezo
Msiulize kwa nini, msijeleta mzozo
Vijana wa themanini, watadoda kama gozo
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

36. Tajeni mahari ndogo, tuweze ilipa yote
Sisi sio wa vigogo, tutawalipa chochote
Mpunguzeni mikogo,muolewe na yeyote
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

37. Wasema wataka chuma, je wewe mwenyewe chuma?
Mdomo umeachama, eti unasaka chuma
Kamuone Muadhama, pia uwe maamuma
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

38. Mambo huwa ni manne, unapotaka kuoa
Hata kama ni mjane, kwanza dini ndio poa
Uzuri jambo lingine, si lazima kwenye ndoa
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

39. Angalia na ukoo, usije ingia chaka
Shauri yako ohoo, jiangalie mkaka
Mali yake mke sio, tafuta yako chalika
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

40. Bado nasema hapana, huko nje kuna Makapi
Hapana tena hapana, hujanielewa wapi?
Naongea ya maana, siniulize wa wapi
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

41. Pita Nyumba tofauti, na kwa Mzee Kigumi
Usiogope umati, wewe fanya kama Mimi
Tafuta wana kamati, sio wale wa umimi
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

42. Sungamile na Shinyanga, kwa Mzee Amrani
Unaweza pata mwanga, pita ukiwa jirani
Usiwe unajivunga, na kuuliza kwa nini
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

43. Nendeni pia Newala, Lajna wamebakia
Hawatasema waala!, ndoa kiwatamkia
Na mpitie Dumila, vimwali wamebakia
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

44. Ntwara waweza kwenda, pia kuulizia
Msisahau Marunda, koo kubwa Tanzania
Watakupikia Ng'onda, siku ukikaribia
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

45. Uingereza si mbaya, jumuia pia ipo
Wala usione haya, kuuliza kama wapo
Na wala sio vibaya, ukamleta ulipo
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

46. Mabinti msichague, mambo huku megeuka
Kama kaja na dengue, ugonjwa unatibika
Wala msijiengue, tupate kufarijika
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

47. Mnauliza salio, mpate kuneemeka
Mtabaki na vilio, siku zikipukutika
Bora mwenye kianzio, ni rahisi kubebeka
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

48. Vumilieni tulivyo, inshallah tatoboa
Ndo mambo ndivyo yalivyo, sione tunawaboa
Jikazeni hivyo hivyo, mbele itakuwa poa
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

49. Pambana na hali yako, binti wa kiislamu
Pigana upate vyako, vya watu huisha hamu
Ndoa na khadim wako, wala hutajilaumu
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

50. Nimefikia mwishoni, kalamu naweka chini
Jifanye hauwaoni, waliokuwa kundini
Unawataka wasuni, uiporomoshe dini
Sioe katu sioe, sioe nje ya kundini
Ukaidi haufai, dunia itakufunza.

Abdallah Said Kalindima (K-Mtoto)
kmtoto1@gmail.com

Kutoka Bwana Shabani hadi Sheikh Shabani

Na RAJABU A. MKIETI

Ni kando kondo ya bahari ya Hindi katika mkoa wa Tanga kaskazini mwa Tanzania utakutana na wilaya ya Mkinga. Ndani ya wilaya hiyo ndio Bwana ATHUMANI KIMPANDA SHUNDA na Bi MWANAIDI MUHAMMED WAMBUA walibahatika kupata mtoto wa kiume siku ya Jumatano 18/3/1992 katika kijiji cha Ng'ombeni. Kwa Fadhila za Allah wazazi wote wawili walikuwa ni Waislamu wa Suni walimpatia mtoto wao jina na kumuita SHABANI ATHUMANI KIMPANDA SHUNDA. Kama nilivyoeleza Baba na Mama walikuwa Waislamu walimlea mtoto wao katika mazingira ya Kiislamu. Mzee Athumani alikuwa akimfundisha kijana wake surat IKLAS kabla ya kulala. Ilipofika wakati wa kumpeleka shule Mzee Athumani alihangaika sana kwani katika kijiji hicho hapakuwa na shule. Mahangaiko hayo yalimfanya mama mmoja katika kijiji hicho kujitolea na kuanzisha shule ya chekechea chini ya mti uitwao MMUMBU na kuanza kupunguza kiu ya Mzee Athumani kwani Mzee Athumani alimpeleka kijana wake katika shule hiyo. Baada ya muda mfupi serikali ilimaliza kiu ya Mzee Athumani baada ya serikali kujenga darasa la makuti kwa ajili ya chekechea. Wanafunzi wote walihamia katika shule hiyo ya serikali, Sheikh SHABANI alimaliza masomo yake ya awali katika shule hiyo ya chekechea ya serikali. Alipomaliza masomo ya awali ililazimika apelekwe kijiji cha Daluni ambako palikuwa na bibi yake Sheikh Shabani ili aanze kusoma darasa la kwanza. Alianza darasa la kwanza katika shule ya Msingi Mkungimize aliweza kusoma mpaka darasa la pili. Baada ya kumaliza darasa la pili Mzee Athumani na Bi Mwanaidi walitengana. Bi Mwanaidi alienda Tanga mjini na Mzee Athumani alihamia kijiji kingine cha Kalalani. Sheikh Shabani aliendelea kukaa kwa bibi yake , kwa hakika maendeleo ya masomo hayakuwa mazuri Mzee Athumani akalazimika amchukue kijana wake huko Kalalani akaendelea na masomo hadi alipomaliza darasa la saba. Mwaka 2007 Sheikh Shabani Shunda alimaliza shule ya msingi. Katika shule hiyo ya Kalalani ni watu wawili tu ndio waliobahatika kujiunga na sekondari mmoja wao ni Sheikh Shabani Shunda. Shule waliofaulu ni shule ya Kata ya Mashewa. Mwaka 2008 Sheikh Shunda alianza kidato cha kwanza na mwaka uliofuata alishindwa kuendelea na masomo ya kidato cha pili. Masomo ya sekondari hayakua mazuri kwa sababu ya hali mbaya ya familia. Wakati fulani Jamaat ilitaka kumuendeleza na masomo ya sekondari lakini msaada ulipofika bwana Shabani alikua ameshahama kijijini . Ikumbukwe Sheikh Shabani akiwa sekondari alishajiunga na Jamaat AHMADIYYA, baada ya hali hiyo bwana Shabani Shunda akaanza kujishughulisha na shughuli mbalimbali za kutafuta kipato.

KUJIUNGA NA JAMAAT

Ipo bishara ya Masihi aliyeahidiwa isemayo (nitafikisha ujumbe wako pembe zote za dunia) Mwanzoni mwa mwaka 2000 Jamaat ilifika katika kijiji cha DALUNI. Juhudi kubwa za mahubiri katika kijiji hicho zilizotimiza bishara hiyo zilifanywa na Dr Nzige, Maulana Sheikh Bakri Kaluta, Mzee Abasi Mkieti, zilifikisha ujumbe huu wa Jamaat katika kijiji cha DALUNI wakati huo ilikua ni wilaya ya MUHEZA kabla ya kugawanywa na kupatikana wilaya ya mkinga. Ikumbukwe kuwa miaka hiyo ndiyo Mzee Athumani alipomleta kijana wake DALUNI ili kusoma shule ya msingi. Maulana Sheikh Bakri Kaluta kila mara alikuwa akienda DALUNI kwa ajili ya malezi na mahubiri. Kipindi hicho bwana Shabani Shunda alikuwa yungali mdogo, yeye na watoto wenzake walikuwa wakikimbiza gari la Sheikh Bakri, mara zote alikuwa akisimamisha gari na kuwachukua watoto wote kwenye gari lake na kwenda nao hadi kwa Mzee Meja Sadara, Ahmadiyya maarufu katika kijiji hicho. Maulana Sheikh Bakri Kaluta alikuwa na mapenzi makubwa kwa watoto kwani chakula alichoandaliwa alikula pamoja na watoto hao, hali hii ilivuta mapenzi ya watoto wengi lakini ilileta mapinduzi makubwa kwa watu katika kijiji hicho kwani wengi waliokuwa wakiichukia Jamaat walianza kupunguza uadui.Ukaribu wa bwana Shabani Shunda na Jamaat uliongezeka zaidi, kwani walimu wa mwanzoni wa Jamaat waliopelekwa katika kijiji hicho walipanga kwenye nyumba ya baba yake kwani watoto wengi walikuwa wakifika nyumbani kwa mwalimu wa Jamaat na katika hali hii walijifunza mambo mengi kuhusu Jamaat ,pia baada ya msikiti wa Jamaat kujengwa katika kijiji hicho walikua wakifika msikiti wa Jamaat na kusali mmoja wa watoto hao alikua bwana Shabani Shunda .

Alipofika darasa la tatu aliachana na mazingira ya kuwa karibu na Jamaat kama nilivyoeleza huko nyuma alichukuliwa na Mzee Athumani huko Kalalani. Katika kijiji hicho alimuacha kaka yake mkubwa bwana Muhammed ambaye baadaye kaka yake alijiunga na Jamaat

Walimu wa Jamaat walikuwa wanabadilishwa kila mara. Aliporudi likizo ya mwaka 2008 mwezi wa tatu alikutana na Mwl Ahmadi Hamisi Majengo baada siku chache bwana Shabani na bwana Haji Mtambuki walienda kwa mwl Ahmadi Majengo ambaye alikuwa mwl wa Jamaat katika kijiji hicho kujiunga na Jamaat. Mwl Ahmadi aliwapatia maelezo machache kuhusu Jamaat baada ya hapo akawapatia baiati fomu na wakajaza kuanzia hapo bwana Shunda akawa amejiunga na Jamaat.



Sheikh Shabani Athumani Shunda

Kama nilivyoeleza mwanzo, Bwana Shabani alishindwa kuendelea na masomo ya sekondari baadaye alirudi Daluni wakati huo alimkuta mwl Abdallah Ramadhani Rundo ndio mwl wa Jamaat katika tawi hilo alikuwa akiendelea kufundisha darasa la watoto katika tawi hilo kila siku baada ya sala ya Magharibi hadi Isha. Bwana Muhameed kaka yake bwana Shabani, alikuwa ameshahamia Tanga mjini alimtumia salamu mdogo wake aanze kusoma katika darasa hilo. Salamu hizo alipozipata mara moja alianza masomo hayo kwa Mwl Abdallah Rundo. Katika darasa hilo bwana Shabani ndio alikuwa mwanafunzi pekee mkubwa. Bwana Shabani alikuwa na uwezo mkubwa kwenye masomo kwani kwa muda mfupi tu alikua tayari ameshamaliza kusoma YASSARNAL QURAN na masomo mengine mengi .

KUJIUNGA NA JAMIA MOROGORO

Mara zote mwl Abdallah alipokuwa akiondoka katika tawi alimuachia majukumu ya kusalisha sala zote. Mwl Abdallah alimjenga bwana Shabani kuwa tayari katika kuitumikia dini kwa wakati wowote . Mwl Abdallah aliona ipo haja ya bwana Shabani kwenda Jamia ya Morogoro ili kuongeza elimu ya dini. Mwl Abdallah alimfikishia wazo hili kaka yake bwana Muhammed na alikubali. Wazo hilo lilifikishwa kwa Sheikh wa Mkoa wa wakati huo, Faridi Tabasamu na aliunga mkono. Mwaka 2009 baada ya Jalsa Salana kulifanyika mitihani wa kudahili wanafunzi wanaojiunga na Jamia ambapo bwana Shabani alikua mmoja wao waliofanya mitihani huo na kufuzu. Alianza masomo ya Jamia Morogoro kwa muda wa miaka mitatu katika miaka yote hiyo bwana Shabani alikuwa akishika nafasi ya kwanza hapo chuoni mpaka alipomaliza. Mwaka 2013 alipomaliza alitunukiwa zawadi ya mwanafunzi bora, sasa bwana Shabani ni mwalimu

SHABANI ATHUMANI KIMPANDA SHUNDA KUJIUNGA NA JAMIA YA GHANA

Mwaka 2013 ulikuwa mwaka usiosahaulika kwani majina ya mwanafunzi wawili yalitakiwa yatajwe ili waende nchini Ghana kwa ajili ya mafunzo ya ubashiri. Muda ulipofika wa kutangaza majina ya wanafunzi wawili wanaokwenda Ghana na jina la Mwl Shabani na Mwl Musa yalitajwa katika Jamia ya Morogoro. Dhifa ya kuwaaga iliandaliwa katika viwanja vya Jamia Morogoro na baaada ya hapo safari ya kwenda Ghana iliandaliwa.

Maandalizi yakakamilika na waliondoka kwa ndege ya Shirika la Ethiopian Airways mpaka Ethiopia kisha wakachukua ndege nyingine kuelekea nchini Ghana. Wakiwa ndani ya ndege Mwl Shabani alimuuliza Mwl Musa kuwa ulishawahi kupata sifuri tangu uzaliwe katika mitihani yako akamjibu hapana. Akamwambia kwa nini tupande ndege na Jamaat imegharamikia tuende kusoma yaani masomo tunayapandia ndege? Mwl Musa akatabasamu. Mwl Musa alikuwa akimkumbusha swahiba wake kwani mambo hayakuwa mepesi huko katika masomo. Wakiwa chuoni huko Ghana walipata changamoto kubwa nayo ilikuwa lugha ya Kiurdu kwa sababu masomo mengi yalifundishwa kwa lugha ya Kiurdu. Walitakiwa wasome miaka saba ila baada ya muda kwa fadhila za Allah mitaala ilibadilishwa kuwa wale waliosoma katika nchi zao miaka mitatu wataendelea kumalizia minne ili iwe miaka saba. Kwa baadhi ya wanafunzi pamoja na Mwl Shabani hali haikuwa nyepesi kwani ilibidi ajifunze zaidi lugha ya Kiurdu usiku na mchana. Ghafla Mwl Musa akaugua sana hali hii ilimpelekea kushindwa kuendelea na masomo kwa mwaka huo. Mwl Shabani akabaki peke yake kwa nchi ya TANZANIA. Hali hii ilimfanya Mwl Shabani apate wasiwasi zaidi na kuongeza juhudi kwani kama asipofanya juhudi akafanikiwa kumaliza siku ya mwisho Tanzania haitatajwa. Kwa Fadhila za Allah aliweza kumaliza na Tanzania ikatajwa akaenda kuchukua Shahada ya kwanza ya Shahid iliyotolewa katika Jamia ya Ghana. Alhamdullilah sasa ni Sheikh SHABANI SHUNDA

Maandalizi ya kuanza kurudi nyumbani yalianza Waliondoka Jamia 4-7-2017 kuelekea Makao Makuu ya Accra na tarehe 5 saa mbili usiku sawa na saa za Ghana waliondoka kupitia Nairobi kisha wakachukua ndege nyingine mpaka Dar es salaam. Siku ya tarehe 6 saa mbili asubuhi ilikua sio ya kusahaulika kwani wanajamaati wakiongozwa na Naibu Amir bwana ISSA MWAKITALIMA walifika uwanja wa ndege kumlaki ndugu MAULANA Sheikh SHABANI ATHUMANI KIMPANDA SHUNDA. Msafara ulianza hapo uwanja wa ndege mpaka Masjid Salaam. Kulifanyika Tafrija ya kukata na shoka . Kuku na chai nzito ya maziwa viliandaliwa kwaajili ya kumlaki ndugu yetu Sheikh Shabani Shunda . Maulana aliulizwa maswali mengi juu ya maendeleo ya masomo yao pamoja na Jamaat ya Ghana Alieleza kuwa Jamaat ya Ghana imeendelea katika kila Nyanja ikiwamo hospitali, shule, vyuo vya ufundi,vyuo vya ualimu,mashamba ya Jamaat ,viwanja vikubwa vya kufanyia mikutano ya kijamaat,misikiti mingi na mikubwa nyumba ya kuishi watumishi,pia wana Jamia mbili ya Mubashirin na Mubalighina na miundombinu kadha wa kadha.

Mwisho

MAKALA ZINAHITAJIKA

Bodi ya Uhariri ya Gazeti letu tulipendalo "Mapenzi ya Mungu" inawaomba ndugu wote kwamba wajitahidi kuleta makala kwa ajili ya kulipamba Gazeti letu.

Ieleweke kwamba Gazeti letu ni la kuelimisha kwa mada mbalimbali. Hivyo kwa kadri mada zinapokuwa nyingi na za kuvutia ndipo litakapokuwa na mvuto zaidi. Pia ni muhimu taarifa mbalimbali zinazotokea Mikoani ziletwe. Kwa wale wote wanaopenda picha zao zitokee kwenye gazeti watuletee nakala ya picha zao.

Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Mapinduzi ya Kujitolea Mali katika njia ya Allah yaliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa

Kutoka Toleo lililopita

Mada iliyotolewa kwenye Jalsa Salana 2017 na:
Sheikh
Abdulrahman M. Ame

"Hii ndio ilikuwa hali ya bidii na shauku kwamba wakati wowote Hadhrat Khalifatul Masihi II (ra) alipotangaza mwanzo wa mwaka mpya wa fedha wa Tahrike Jadid, kati ya wa mwanzo kuahidi ahadi za Mwaka Mpya walikuwa ni marafiki wawili. Wa kwanza alikuwa ni Muhammad Ramzān Sahib, aliyekuwa karani, na mwingine Muhammad Boota Sahib, aliyekuwa dereva wa gari la farasi. Kwa muda wote wawili hawa walipokuwa hai kamwe hawakukubali kubaki nyuma [katika kuwa wa kwanza kutuma ahadi zao]. Walifanya ahadi zao kwa mujibu wa nguvu ambazo Allah Alikuwa Amewapa nao pia walikuwa kati ya wa mwanzo kulipa ahadi zao. Na muda wote walikuwa wa kwanza kwenda kusubiria mbele ya ofisi ya Katibu Mukhtasi (kwa siku hizo watu walikuwa wanakwenda kwenye ofisi ya Katibu mukhtasi [kwa ajili ya kulipa ahadi zao]). Hali ya wafanyakazi ilikuwa kiasi hiki kwamba mfanyakazi mmoja kutoka Sialkot ambaye alikuwa akipata rupia mbili tu kwa siku iliahidi kulipa rupia 30 katika mchango huu. Mtu mwingine, ambaye alikuwa pia maskini, aliahidi rupia 10. Kama hivyo, ndivyo ilivyokuwa hali ya wale waliojitoa mhanga."

Mpango wa Tahrik Jadid ni mmoja tu lakini mipango hii iko kadhaa. Waqfu Jadid, Ujenzi wa Misikiti, Mradi wa kutafsiri na kuchapisha Qurani Tukufu katika lugha mbalimbali, uchapishwaji wa Magazeti, MTA, n.k. Bila kusahau michango mikuu na ya lazima (Chanda Aam, Chanda Wasia, Chanda Jalsa Salana, Tanzeem) hii yote iwapo utapitia kurasa za historia zake inayo matukio ya kusisimua imani ya mtu kwa kiwango cha kumfufua aliyekufa.

Hapa pia nitaje mifano michache katika baadhi ya michango hii

1. Katika Miradi ya ujenzi wa Misikiti; Mnamo mwaka 1920, wakati Hadrat Khalifatul Masih II (ra) alipowaomba Lajna Imaillah wajitokeze kuchangia fedha kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa Berlin nchini Ujerumani. Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. alitoa pongezi yeye mwenyewe juu ya muitikio ulivyokuwa mkubwa akisema:

"Mnamo mwaka 1920 hali ya Jamaat ilikuwa hivi kwamba wakati nilipoomba mchango wa Rupia 100,000 kutoka kwa kinamama kwa ajili ya Ujenzi wa Berlin Mosque, Kinamama wa Jumuiya walichangia kiasi hicho ndani ya mwezi mmoja tu. Walivua mapambo yao na kuyauza kutimiza lengo hili. Wakati ambapo katika watu wengine hali ni hii kwamba watu hufikia kuritadi wanapoambiwa wajitolee kifedha, hapa tunao mfano wa kipekee, kwamba niliomba msikiti huu ujengwe na kinamama wa Kiahmadiyya kama zawadi kutoka kwao kwa ajili ya ndugu zao wa Ujerumani. Sasa badala ya kuwa, kinamama hawa ambao kwa kawaida huonekana dhaifu, warudi nyuma baada ya kusikia mpango huu, Kinyume chake tumeona hali ya kuvutia zaidi....

Hadrat Khalifatul Masih IV (rh) katika hotuba yake ya tarehe 12, Septemba 1992 kwenye Jalsa Salana ya Ujerumani, akitaja kujitolea walikokufanya kinamama kwa ajili ya msikiti huo alisema:

"Hadrat Fadle Umar [Khalifatul Masih II (ra)] alitaja kujitolea kwa mama mmoja Mwanajamaat wa Kipakhtoon. Alikuwa ni mama mzee ambaye hawezi hata kutembea vizuri. Alikuja kwangu na kuweka rupia mbili mkononi mwangu. Mama huyu alikuwa ni maskini kiasi hiki kwamba alikuwa akiishi kwa msaada wa Jamaat. (Nilipomueleza kwamba yeye anaishi kwa msaada wa Jamaat), Mama huyo alikamata mtandio wake na kusema huu unatoka kwenye Jumuiya. Akakamata kanzu yake na kusema hii inatoka kwenye Jamaat, Akaonyesha viatu vyake navyo akasema vinatoka kwenye Jamaat. Posho yake ya matumizi pia inatoka kwenye Jamaat. Akasema rupia mbili hizi pia zinatoka kwenye Jamaat, nilizidunduliza kwa haja yangu fulani, lakini nazitoa kwa ajili ya Jamaat. Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. akasema: Ni kubwa kiasi gani ilikuwa jazba yake.

Yule mama akaendelea kusema Quran yangu pia inatoka kwenye Jamaat. Mimi mwenyewe sina chochote cha kwangu, Ninapata kila kitu kutoka Jamaat.

Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. anasema: Wakati anasema haya kila neno lilikuwa likiukata moyo wangu kama upanga huku moyo wangu ukibubujikwa na shukurani, nikimkumbuka yule mhisani Mkuu (Masihi Aliyeahidiwa a.s.) ambaye amezipatia uhai wa kijani kibichi roho za taifa ambalo lilikuwa limekufa. Na sauti hii ilikuwa ikitoka ndani mwangu kwamba: Ee Mola wangu, ni mkuu kiasi gani Masihi wako ambaye amezibadilisha nyoyo za hawa Wapakhtoon, ambao hapo kabla walikuwa wakiiba kutoka kwa wengine lakini leo wanaona heshima kutoa muhanga kwa ajili ya taifa lao, jamaa zao na kujitolea mali kwa ajili ya dini Yako!

Katika michango ya ujenzi wa msikiti huu mabibi kadhaa walijitolea kiasi kikubwa: Kwa mfano Hadhrat Sayyeda Nusrat Jehan Begum alijitolea Rupia 500 alizozipata kwa kuuza mali yake. Fedha zote alizopata kwa mauzo hayo alizitoa katika njia ya Allah.

Hadhrat Sayyeda Nawab Mubarika begum Sahiba alijitolea rupia 1000. Hivyo hivyo, Hadhrat Nawab Amatul Hafeez begum sahiba, mke wa Mirza Sharif Ahmad Sahib, mke wa Mir Muhammad Ishāq Sahib, na mke wa Mirza Sultan Ahmad Sahib, wote hao walijitolea kwa kiasi kikubwa sana. Hadhrat Sayyeda Amatul Hayee Sahiba alitoa mchango mkubwa wa fedha na Hadhrat Sayyeda Umme Tahir alitoa mapambo yake na fedha pia.


Sheikh Abdulrahman M. Ame

Si hao tu ambao wanaweza kusemwa kwamba uwezo wao ulikuwa mkubwa kidogo lakini hata wale walioonekana maskini kabisa hawakukubali kubaki nyuma:

Mama mwingine wa Kipakhtoon ambaye alikuwa mhamiaji huko Qadian ambaye pia alikuwa hawezi kutembea bila msaada alikuja kwa Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. na kutoa rupia 200. Mama huyu alikuwa ni maskini kiasi hiki kwamba alikuwa anamiliki kuku 4 tu na alikuwa akiishi kwa kuuza mayai yao, na ili kukidhi mahitaji yake mengine alikuwa akiishi kwa msaada wa Jamaat. Mama mmoja wa Kipanjabi alijitolea mapambo yake ambayo yalikuwa ni hayo tu, kwa ajili ya ujenzi wa msikiti huu. Mama mmoja aliyefiwa na mumewe na ambaye alikuwa akiwaangalia mayatima, alitoa vifaa vyake vyote vya nyumbani ambavyo alikuwa anavimiliki kwa ajili ya matumizi yake. Mke wa rafiki mmoja kutoka Bhagalpur alikuja na mbuzi wawili na akasema huu tu ndio mchango tulionao, tunaomba uupokee.

Kwa kuzingatia Fadhili za Allah katika nyakati ngumu, Hadrat Khalifatul Masih II (ra) alianzisha mchango kwa ajili ya ujenzi wa msikiti wa London. Alitaka rupia 30,000 zichangwe kwa ajili hiyo. Kwa lengo hilo aliongea na kinamama baada ya sala ya Alfajr tarehe 7 Januari na akaongea na kinababa siku ya Ijumaa tarehe 9 Januari. Mpaka ilipofika tarehe 11 Januari jumla ya rupia 12,000 zilishachangwa. Akieleza shukurani zake na kufurahishwa kwake kwa mchango huu Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. anasema: Mchango wa kiwango hiki kutoka Jamaat hii iliyo maskini hakuwezi kuwa kingine chochote zaidi ya msaada wa Allah. Ninaamini kwamba Baraka za Allah zipo pamoja na mchango huu. Katika siku hizo jazba ya wanajamaat wa Qadian ilikuwa inapendeza kuiona. Ni wale tu ambao waliweza kuiona kwa macho yao ndio wanaoweza kuielewa. Wanaume, wanawake na watoto wote walionekana kuelemewa na mapenzi (ya kujitolea). Kinamama wengi walitoa mapambo yao kama mchango. Wengi walijitolea na kisha wakapatwa tena na hamu ya kujitolea mara nyingine na wakatoa kwa majina ya watoto wao. Hawakuridhika na hilo tu bali walianza kujitolea kwa majina ya jamaa zao waliokwisha fariki...

Mtu mmoja aliniandikia kwamba kutokana na umaskini alionao hawezi kujitolea kiasi kikubwa, hata hivyo kwa msisitizo mkubwa sana aliniomba akisema kwamba mimi sina zaidi cha kujitolea ila naomba ukubali kuipiga mnada duka yangu na chochote kitakachopatikana kiwe ni mchango wangu kwa ajili ya ujenzi wa msikiti huu.

Kuhusu uanzishwaji wa Mgazeti:

Gazeti la Al-Fadhl lilianzishwa mwaka 1913. Kuanzishwa kwake pia ni hadithi ya kusisimua. Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. pia analieleza hili kwa maneno yake: Allah Mtukuka Aliingiza wazo hili ndani ya moyo wa mke wangu kama vile Alivyoliingiza kwenye moyo wa Hadhrat Khadija katika kumsaidia Mtukufu Mtume s.a.w. Yeye (mke wangu) kwa kuelewa kwamba kuwekeza fedha kwenye gazeti ni sawa na kuzimimina fedha kwenye mto, na hasa kwa gazeti lile ambalo mwanzilishi wake ni Mahmood, ambaye inawezekana ni mtu aliye maarufu kwa wakati huo. Pamoja na hayo alijitolea seti mbili za mapambo yake na akanipatia ili ziuzwe na fedha itakayopatikana itumike kuanzisha gazeti. Seti moja ya mapambo hayo ilikuwa ni mali yake binafsi na seti moja ilikuwa ni mapambo yake ya tangu utotoni ambayo aliyahifadhi kwa ajili ya binti yake, Nasira Begum. Niliyapokea mapambo hayo na kuelekea Lahore muda huo huo na kuyauza kwa Rupia 475. Hizi zilkuwa ndio fedha za kuanzisha Gazeti la Al-Fadhl. Gazeti la Al-Fadhl litaendelea kuhuisha kumbukumbu za unyonge wangu na kujitolea kwa mke wangu. Ni ukweli ulioje, kinamama walivyo wafanyakazi wa kimya kimya...

2. Miradi ya kufasiri Quran Tukufu.

Wakati ilipotangazwa mpango wa kutafsiri na kuchapisha Kurani tukufu kwa lugha mbalimbali, Hadhrat Khalifatul Masih II r.a. hapo tareher 20, Oktoba 1944, alizipangia Jamaat mbalimbali kulipia tafsiri ya lugha fulani, lakini pamoja na hayo wapo watu binafsi kadhaa waliojitokeza na kudhamini wao wenyewe tafsiri fulani: kwa kuwataja wachache

1. Hadrat Khalifatul Masih II (ra) mwenywe -- Kitaliana
2. Hadrat Khalifatul Masih IV (rh) - Kichina
3. Chaudhry Zafrullah Khan (ra) - Lugha moja yoyote n.k.

Hiyo ni baadhi ya mipango makhasusi tu lakini kila shida fulani ilipotokea na wanajamaat wakatakiwa kujitolea walijitokeza mbele kwa moyo wa ajabu.

Leo, Alhamdulillah, Jamaat Ahmadiyya inao utaratibu na mpangilio wa utoaji katika njia ya Allah kwa namna ambayo hakuna taasisi yoyote, bali tunaweza kusema hata serikali yoyote ya dunia ambayo inaweza kuonesha mfano wake.

Kila mwaka, kila mwezi, bali kila siku, kila saa na dakika ipitiyo duniani Waahmadiyya kwa njia moja au nyingine katika kona zote za dunia wanaonyesha mifano ya kujitolea inayodhihirisha mapinduzi makubwa yaliyotokea ndani yao.

Hapa naomba nitoe mifano michache iliyotokea nje ya Bara Hindi ili asije akadhani mwenye kudhani kwamba mti huu uliota kwenye udongo wa aina moja tu labda kwa habati nasibu.

Hadrat Khalifatul Masih V (aba) akitaja baraka za Allah katika kujitolea mali katika hotuba yake ya Jalsa Salana ya UK mwaka 2003, alitaja matukio machache ya kuchangia ujenzi wa misikiti kwa maneno yafuatayo:

"Jibreel Saeed, Mbashiri wetu wa Ghana anaandika kwamba nilikwenda kuitembela Togo nikiwa na rafiki yangu mmoja Al-Hajj Muhammad Agboobey. Tulisali sala ya Adhuhuri mahala paitwapo Najong mahala pa wazi jua likiwa kali. Al-Hajj Muhammad Agboobey akasema watu hawa wanastahili tuwajengee msikiti. Hiki kilikuwa ni kijiji kidogo tena cha wanajamaat wapya, hivyo akajitolea mchango mkubwa kujenga msikiti mzuri hapo. Msikiti aliojenga unaingia watu 300, na ingawaje kijiji hiki kiko ndani sana na usafiri ni mgumu lakini alisafirisha vifaa kwa hali ngumu na ghali.

Mbashiri wetu wa Kazakhstan anaandika kuhusu mwanajamaat mpya aliyejitolea kiwanja chake kwa ajili ya kujenga msikiti wa Jamaat. Kwenye kiwanja hicho kuna nyumba ya gorofa moja pia. Zaidi ya hayo alinunua kiwanja kingine kwa ajili ya msikiti kwenye mji mwingine. Pamoja na kwamba ni Mwanajamaat mpya lakini amejitolea jumla ya USD 495,000

Ndugu Wasikilizaji hili hapa ni tukio la kusisimua la kujitolea mali bali la kuonyesha jinsi mtu aliyekuwa mgumu kabisa alivyobadilika kwa kumkubali Masihi Aliyeahidiwa a.s. na akawa mtoaji mkubwa, nalo linahusu uanzishwaji wa Ahmadiyya Press ya kwanza huko Sierra Leone.

Wakati Jumuiya ilipoanzisha gazeti huko Sierra Leone, kwa vile hatukuwa na Printing Press yetu, ilibidi kulichapisha gazeti hilo katika kiwanda cha

Endelea uk 9

Mapinduzi ya Kujitolea Mali katika njia ya Allah yaliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa

Kutoka uk. 8

uchapishaji cha Wakristo. Mwanzoni walituvumilia lakini baada ya matoleo matatu au manne hivi, jopo la wachungaji lilimwendea mmiliki wa kiwanda hicho na kumwambia huna hata aibu, unawachapia Waahmadiyya gazeti lao wakati unajua ni sawa na kuupiga shoka mzizi wa Ukiristo. Hivyo mmiliki wa kiwanda akapata jazba na akasema kuanzia hapo hatochapa tena gazeti letu kwa sababu wachungaji hawakubaliani na jambo hilo. Wakati kiwanda hiki kilipokataa kuchapisha gazeti letu Wakristo wakafurahi sana na wakatangaza kwenye gazeti lao kwamba tumezuia kuchapisha gazeti la Waahmadiyya, na sasa tutaona jinsi Mungu wa Islam Atakavyowasaidia. Wakasema tulikuwa tunawachapishia, lakini sasa hatuwachapishii tena, na wao hawana mashine wala kiwanda cha uchapishaji, sasa tutaona Mungu wa Islam Atawasaidiaje iwapo Anazo nguvu za Kuwasaidia dhidi ya Kristo.

Kwa kusoma hayo Mbashiri wetu Maulana Muhammad Siddiq Sahib Amritsari akapata maumivu makubwa ya moyo na akajisemea kwamba Jamaat hapa ni ndogo lakini sina watu wengine wa kuwaeleza jambo hili isipokuwa Wanajamaat hawahawa. Hivyo akanunua tiketi ya Lori na akasafiri kilomita 275 hadi kijiji fulani ambako Mwanajamaat mpya ambaye pia ni Chifu wa kijiji hicho alikuwa anaishi. Chifu huyu kabla ya kujiunga alikuwa mpinzani mkubwa wa Jumuiya na alikuwa akisema kwamba maji yanaweza kupanda mlima lakini yeye hawezi kamwe kujiunga na Ahmadiyya. Lakini kwa shani ya Allah Chifu huyu sio tu alijiunga bali akabadilika na kuwa mtoaji mkubwa sana katika njia ya Allah. Pia ikatokezea kwa Fadhili za Allah kwenye ardhi yake ikagundulika Almasi na ingawaje sheria ya nchi hiyo ni kwamba madini yote ni mali ya umma, lakini alilipwa kiasi kikubwa kama fidia kwa ajili ya ardhi ambayo ilikuwa itumike kwenye uchimbaji huo. Hivyo mara tu alipolipwa alitoa mchango wa Paundi 500.

> *Je hatupo baadhi yetu ambao tuendapo kwa katibu wa fedha hatutaji mapato yetu halisi badala yake husema tu bwana ndio hicho hicho nikatie michango yote kama ujuavyo?*

Akiwa njiani kama maili 8 kutoka kijijini kwake, Mbashiri wetu alimuona Chifu huyo akiwa kwenye lori lingine akielekea mahala fulani kwa haja binafsi. Chifu naye alipomuona Mbashiri wetu akashuka kwenye lori na kumkimbilia, huku akimuuliza ni nini kilichomleta kule muda huo. Mbashiri wetu akamhadithia hadithi yote na kumuomba achangie fedha ili waweze kununua mashine za kwao kwa ajili ya uchapishaji wa gazeti. Kusikia hivyo chifu yule pale pale akamwambia Mbashiri wetu nisubiri hapa hapa naye akarudi kijijini kwake na aliporudi akamkabidhi paundi zingine 500 na kumuomba ajitahidi ili waweze kuwa na kiwanda chao cha uchapishaji haraka iwezekanavyo ili waweze kuwajibu Wakristo kwamba ingawaje mmetukatalia kutuchapishia gazeti letu katika kiwanda chenu lakini Mola wetu ameturuzuku kiwanda cha kwetu wenyewe. Paundi 1000 kilikuwa ni kiwango kikubwa cha fedha wakati huo ambapo hata mfanya biashara mkubwa asingeweza kutoa kiasi hicho kwa mara moja.

Baada ya kupata kiasi hicho Mbashiri wetu anasema akamwendea Mfanyabiashara mmoja Mwanajamaat mwenye asili ya Syria na kumueleza kwamba Chifu fulani wa kijijini amechangia paundi 500 kwa lengo la kuanzisha kiwanda cha uchapishaji hivyo na yeye achangie chochote. Ndugu huyu akasema nami nachangia paundi 500, na akasema sitokubali kushindwa na Chifu wa kijijini, Inshallah nitachangia zaidi siku zijazo.

Mbashiri wetu anaendelea kuhadithia kwamba baada ya kuchangia fedha hizo na watu wengine nao wakajitolea aliendelea kupata hofu kila siku zilivyokwenda ni wapi na kwenye jengo gani wataweza kuanzisha kiwanda hicho. Kwa wakati huo Jamaat ilikuwa na Mission house katika mji wa Bo tu. Usiku mmoja wakati akijigeuza geuza kitandani kwa tafakuri akamuomba Allah Awasaidie juu ya mahala pa kuanzisha kiwanda hicho. Ghafla akapata wazo la kumwendea Mwanajamat mmoja tajiri Al-Haj Ali Rogers sahib ili amuombe ajitolee nyumba zake mbili zilizokuwepo kwenye kiwanja kimoja katikati ya mji wa Bo ili zitumike kwa ajili ya Press.

Mbashiri wetu anasema, asubuhi na mapema alimtembelea Al-Haj Ali Rogers sahib na alimueleza juu ya wazo hilo na kumtaka ajitolee nyumba zake mbili pamoja na ardhi iliyokuwa pembezoni mwake ili zitumike kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha uchapishaji cha Jamaat. Anasema moyo wake ulipatwa na mshangao wa ajabu kwamba hapo hapo na bila kupepesa maneno Al-Haj Ali Rogers sahib aliniambia yote uliyoomba nimeyakubali na sasa hivi lete karatasi ili niandike mkataba wa kuzitoa nyumba zangu kwa ajili ya Jamaat. Mkataba ukaandikwa na nyumba hizo pamoja kiwanja cha pembezoni mwake ambavyo vilikuwa na thamani ya Paundi 3000 kwa wakati huo akavitoa kwa ajili ya Jamaat. Pamoja na nyumba hizo na kiwanja chake Al-Haj Ali Rogers sahib yeye na familia yake wakajitolea paundi zingine 500 ili zisaidie kwenye ununuzi wa mashine za Press. Mbali ya kufungua kiwanda nyumba hizo pia zikatumika kuanzisha Maktaba ya Jamaat.

Ni ajabu tupu mapinduzi haya!

Ndugu wasikilizaji,

Mifano hii yote niliyoitaja ni ya nchi mbalimbali duniani, na sijataja mfano wowote wa hapa kwetu, lakini hii isidhaniwe kwamba hapa kwetu watu hawajapata mapinduzi ya kujitolea katika njia ya Allah.

Hapa kwetu pamoja na hali za wanajamaat wengi kuwa duni lakini sawa na hali zao wamejitolea vya kutosha:

Viwanja kadhaa ambavyo misikiti ya Jamaat imejengwa: vijijini na hata mijini vilitolewa na wanajamaat kwa mapenzi yao wakiiomba Jamaat ikubali sadaka yao kwa furaha.

Msikiti wetu wa Kivule - Dar es Salaam. Mengwa, Mkongo, Kibaha na Kitanga - Pwani. Dhutumi, Mkami na Kibwaya - Morogoro. Kilanje Lanje - Lindi. Mtama, Mahuta - Mtwara. Kilungu, Igoko na Mwakashinde - Tabora, bila kuusahau msikiti wetu wa mjini Mwanza tusaliao kwa sasa ni mifano tu ya viwanja kadhaa ambavyo wanajamaat wa Tanzania wamejitolea katika njia ya Allah.

Nadhani utajo huu wa kujitolea hapa kwetu utakuwa na deni kubwa iwapo sikuwakumbusha ndugu zangu wasikilizaji kwamba hata hapa tulipokaa sasa napo pametokana na baraka ya kujitolea katika njia Allah, pale ambapo mzee wetu mmoja. Bw. Sultani Ungando alipotoa ardhi yake yenye ukubwa wa takriban ekari tano ili itumike kwa ajili ya kujenga shule ya Jamaat. Ni hapo baada ya Jamaat kuikubali sadaka yake hiyo ndipo wazo la kupanua eneo hili lilipokuja na baada ya kuongeza upana na urefu wa eneo letu ikaonekana sio shule tu bali hata Shura na Jalsa vinaweza kufanyika hapa.

Ndugu zangu wapendwa nimalizie hotuba yangu kwa kujitanabahisha mimi mwenyewe na kuwakumbusha nanyi pia kwamba:

Mola wetu si Mola mhitaji wa chochote kutoka kwetu. Yeye ni ***Ghaniyyu*** na sisi ni *Fuqaraa*.

Hata kama hali yetu ionekane duni vipi, Yeye ni Muweza wa Kuibadilisha siku Atakayo na saa Atakayo na kwa namna Atakayo.

Alhamdulillah, baadhi yetu tunajitolea kiasi, lakini bado baadhi yetu ni kana kwamba tunamfanyia mzaha Mungu ambaye anaturuzuku kumi nasi tunaiambia Jamaat kwamba sisi tunachoruzukiwa hatujui ni kitu gani? Je hatupo baadhi yetu ambao tuendapo kwa katibu wa fedha hatutaji mapato yetu halisi badala yake husema tu bwana ndio hicho hicho nikatie michango yote kama ujuavyo. Na je hatupo miongoni mwetu ambao katika kuandaa bajeti ya mwaka hatukubali kutaja mishahara yetu hata siku moja tukidai kwamba mshahara ni siri ya mtu. Na iwe hivyo kuwa mshahara ni siri ya mtu, je siri hiyo unataka kumficha hata Mungu na Khalifa wake? Je yule anayemfanyia Mungu mzaha wa kiasi hiki anatarajia alipwe nini tena zaidi ya mzaha!

Kisha tupo miongoni mwetu ambao tunamsuta Allah kwa kuiambia Jamaat kwamba sisi Mungu haturuzuku chochote, kwa muda wa miezi sita. Je hatupo hapa baadhi yetu ambao kwa muda wa miezi sita hatujatoa chochote? Je hapo tena tunamtarajia Mungu Atufanyie nini tena zaidi ya Yeye kutusuta nasi.

Kisha kuna hatari itishayo zaidi ifanywayo na baadhi yetu pale tunaponeemeshwa na Allah, hata kama hapo kabla tuligaragara kwenye sakafu za *Masjid Salaam*, Dar es Salaam au *Masjid Fazal* Tabora, au *Masjid Ihsan* Songea n.k., huku tukiwaomba Wabashiri wetu na wazee wetu jamani mtuombee vijana wenu, lakini mara tuneemeshwapo tunajisahau, tunadharau, tunakejeli bali tunakuwa kama *Thaalaba*, na kusema, nini hii Jumuiya nayo inataka kodi! Kisha nini basi tunakitegemea kutoka kwa Allah zaidi ya kutujibu nami sikutakeni basi, na sitaki kujitolea kwenu kokote na sitaki kusikia maombi yenu wala kilio chenu! Watu wa aina hii hatimae hutupwa nje ya Jamaat! Watu wa aina hii ni mkosi mkubwa kwa ajili ya Jamaat, ni kana kwamba wanamfanya Mungu Aushangae uwezo wetu '*Watanzania*' kwamba hatuna sifa ya kubeba neema za Mungu na hivyo ili kutunusuru tusije tukaanguka sote moja kwa moja, basi labda wengine tusaidiwe kwa kuachwa kuendelea kusota daima.

Hii ndio hali ya baadhi yetu, na aliimba kweli muimbaji Khamisi Wamwera aliposema:

Anayo nyumba ya mawe, ana gari za selera
Ana mashamba Kongowe, na duka za biashara
Anafuga na wenziwe, ng'ombe, mbuzi na sungura
Kutowa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani!

Kwa umbo na kwa taswira, si kama mimi na wewe
Wajihi wake wang'ara, umestawi mwiliwe
Akivaa wastara, ni yeye atambuliwe
Kutowa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani!

Afadhali na ajuwe, neema hiyo fundira
Amepewa na Molawe, si akili si busara
Akakumbuka atowe, fungu la Mola Qahara
Kutowa mali kwa Allah, kumekuwa mtihani!

Ndugu zangu wapendwa, mwaka huu kwenye shura yetu tulimuahidi Huzur Aqdas kwamba tutapunguza utegemezi wa bajeti yetu kwa asilimia 5 kila mwaka kuanzia mwaka huu. Hii si ndoto tusiyoweza kuitimiza. Hebu tusimame sote kwa pamoja, hebu tusimame kwa ukweli wa nyoyo zetu zote, hebu tuondowe mapenzi ya mali ndani ya nyoyo zetu, hebu tumkimbilie Mola wetu, kisha tuishuhudie dunia ikitukimbilia nasi kwa kasi.

Allah Atusaidie kuyaelewa haya na kuyatekeleza! Amin.

ASEMAVYO MASIHI ALIYEHIDIWA

Wamebarikiwa wafungwa wale waombao dua bila ya kuchoka, kwani siku moja watafunguliwa.

Wamebarikiwa vipofu wale wasio wavivu katika kuomba dua, kwani siku moja wataanza kuona.

Wamebarikiwa wale waliomo makaburini wakifanya maombi kuomba msaada wa Mungu, kwa sababu siku moja watatolewa nje kutoka makaburini.

Mmebarikiwa ninyi msipochoka hata kidogo kuomba dua, na roho zenu zinayeyuka kwa ajili ya maombi na macho yenu yanatiririsha machozi na kuzalisha moto fulani ndani ya vifua vyenu na kuwapelekeni ndani ya vyumba vyenye kiza na misitu pasipo watu kwa ajili ya kuipata ladha ya kuwa upwekeni na kuwafanyeni kuwa wenye kukosa utulivu, wenye kelemewa na mapenzi na kuwa kama mliochanganyikiwa, kwani hatimaye mtafadhiliwa. Yule Mungu tunayeitia Kwake ni Mkarimu na Mrahimu mno, Mwenye haya, Mkweli, Mwaminifu, Mwenye kuwahurumia wanyonge. Basi nanyi pia kuweni waaminifu na ombeni dua kwa ikhlasi na uaminifu kamili, hivyo Yeye Atawarehemuni. Jitengeni na vurugu za dunia, na magomvi ya nafsi msiyafanya kuwa ya kidini.

Jichagulieni ushinde, na kubalini kushindwa ili mkawe warithi wa maushindi makubwa makubwa. Mungu Atawaonyesha mwujiza waombao dua, na waombao watapewa neema ya kimwujiza.Dua hutoka kwa Mungu na kuelekea huko huko Kwa Mungu. Kutokana na dua Mungu Anakuwa karibu kama vile roho yenu ilivyo karibu nanyi. Neema ya kwanza ya dua ni kwamba mabadiliko matakatifu huzalika ndani ya mwanadamu, halafu utokana na mabadiliko haya Mungu pia Hufanya abadiliko katika sifa Zake. Na sifa Zake si zenye kubadilika lakini kwa ajili ya mwenye kubadilika kunakuwa na mdhihirisho mmoja tofauti ambao dunia haiufahamu, kana kwamba Yu Mungu mwingine ilhali hakuna Mungu mwingine yeyote yule, lakini mdhihirisho mpya unamdhihirisha kwa namna mpya. Ndipo katika shani ya mdhihirisho huo makhsus Humtendea yule aliyebadilika yale ambayo Hawatendei wengine.

Huu huu ndio ule mwujiza.

Kutoa Katika Njia ya Mwenyezi Mungu

Kutoka uk. 12

wake. Kwa hakika elimu na Afya ni vitu vilivyopewa umuhimu mkubwa katika Islamu. Mtume Mtukufu s.a.w. akasema:- " Tafuteni elimu hata kwa kwenda uchina." Tena akasema kuhusu tiba: " Hakuna ugonjwa wowote ila Mwenyezi Mungu ameumba na Dawa yake isipokuwa mauti."

4 SHUKURANI: Ni aina ya mchango unaotolewa na Mtu baada ya kutoka kwenye matatizo, tabu na shida. Pia mchango unaotolewa na mtu baada ya kupata mavuno, upo katika kipengele cha shukurani. Tunasoma ndani ya Kur`an Tukufu juu ya jambo hili Mwenyezi Mungu kaagiza :-"Kuleni matunda yake ipambapo, na toweni haki yake siku ya kuvunwa kwake" (6:142)

5 FIDIA: Ni aina ya mchango unaotolewa na mtu ambaye kwa udhuru halali ameshindwa kutekeleza amri fulani. Mfano hai juu ya mchango huu upo ndani ya Kur`an Tukufu inapoeleza juu ya watu waliokosa kufunga saumu kwa ajili ya kuumwa au kusafiri. Tunasoma:-" Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku nyingine. Na wale wanaoweza, basi watoe fidia kwa kuwalisha masikini. (2:185)

6 KAFARA: Hii ni aina ya mchango unaotolewa kama adhabu baada ya mtu kufanya kosa. Kwa mujibu wa Kur`an Tukufu kuna makosa ambayo yamewekewa kanuni ya adhabu hapa hapa duniani. Kwa mfano mtu anaposhindwa kuchunga ulimi wake hadi akafikia kumwambia mke wake kuwa ni mama yake. Hilo ni miongoni mwa makosa ambayo Mwenyezi Mungu ameyawekea kanuni ya adhabu hapa hapa duniani. Katika kukomesha jambo hilo Mwenyezi Mungu anasema:- "Na wale wawaitao wakezao mama, kisha wakarudia katika yale makosa waliyoyasema, basi wampe mtumwa uhuru kabla ya kugusana. Na asiyeweza basi alishe masikini sitini". (58:4-5)

7 HUDUMA ZA FAMILIA: Mtu anapoihudumia vizuri familia yake kwa kuipatia mahitaji ya lazima sawa na uwezo wake, kwani kitendo hicho ni miongoni mwa Amri za Mwenyezi Mungu; kama anavyosema:-" Na wanawake walio zaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kwa anayetaka kukamilisha. Na ni juu ya baba yake (kutoa) chakula chao na nguo zao kisheria"(2:234).

8 KULIPA MISHAHARA YA WATUMISHI: Mtu anapo ajiri watumishi naye akalipa mishahara kwa watumishi wake baada ya kufanyia kazi sawa na mkataba wao, Jambo hilo pia linahesabiwa kuwa ibada ya mali. Kiongozi wetu Mtume Muhammad s.a.w. anasema; "Mpe kibarua ujira wake,kabla halijakauka jasho lake"

9 KUTOA HUDUMA KWA WAZAZI: Kuwahudumia wazazi kwa kuwapa mahitaji ya lazima ni mojawapo ya kazi njema ambazo mbele yake mwenyezimungu huhesabiwa kuwa ibada. Kwa hakika wazazi wamekuwa ni njia ambayo mtu amepita wakati wa kuja duniani. Ndio maana Mwenyezi Mungu Amesistiza sana kuwahurumia na kuwasaidia wazazi. Hebu rejea aya " Na mola wako ameagiza kuwa usimwabudu yeyote ila yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi kama mmoja wao akifikia uzee pamoja nawe, au wote wawili basiusiwaambie hata Akha, wala usiwakemee,na usemenao kwa msemo wa heshima. Na uwainikie bawa la unyenyekevu kwa huruma. Na useme mola wangu uwarehemu kama walivyonilea katika utoto.(17:24-25).

10 KUTOA ZAWADI: Mtu anpotoa zawadi kumpa mwenzake, basi kitendo hicho nacho kinatambuliwa kuwa ni sehemu ya ibada; kwani kinaongeza mapenzi baina ya atowayo na anayepewa. Kwa kulifahamu jambo hilo, Mtukufu Mtume wetu s.a.w amesema kwamba:-" peaneni zawadi mpendane"

Hiyo hapo juu ni baadhi tu ya vipengele ambavyo mtu anapotoa mchango kulingana na vipengele hivyo huhesabiwa kuwa anatoa katika njia ya Mwenyezimungu. Katika Jamati yetu ya Ahmadiyya tuna utaratibu wakutoa michango ya Wasia, Kawaida, Tahrik Jadidi, Wakfu Jadidi, n.k. hiyo yote ni michango inayotolewa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Kwakuzingatia umuhimu wa kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu, Mwanzilishi mtukufu wa Jamati Ahmadiyya ameagiza :- "Na Jamati mzima inawajibika kutoa msaada kwa mwendeleo huu katika kila hali. Vile vile kusiwe na ulegevu wowote katika kutoa misaada kifedha. Angalieni kwamba hakuna mwendeleo wowote duniani ambao unaweza kuendelea bila michango. Michango ilikuwa ikikusanywa wakati wa Mtume s.a.w. nabii Mussa a.s na halikadhalika wakati wa Nabii Issa a.s hawa wote walikuwa ni Mitume wa Mwenyezi Mungu. Hivyo basi wanachama wa Jamati yetu inawalazimu waliangalie sana jambo hili. Mengi yanaweza kutendeka iwapo kila mwanajumuiya atatoa michango yake bila kukosa. Lakini kama itatokea mmoja hatoi michango yake, kuna faida gani kwa mtu kama huyo kubaki ndani ya jamati? Mwendeleo unahitaji sana msaada wa fedha wakati huu.

Kama mtu anakwenda dukani, hutumia fedha nyingi kwa kuwanunulia watoto wake mabandia (toiys) basi kuna madhara gani yatakayompata kama atatumia senti yake kwakutoa Michango? Matumizi Mengi yamefanywa kwa kununua nguo, chakula na mahitaji mengine mengi. Kwanini basi kunafikiriwa kutumia fedha kwa matumizi ya dini kuwa ni mzigo?..

Kila mwanajumuiya wa Jamaati yetu anawajibika kutoa ahadi kwa dhati na kulipa kiasi fulani cha fedha kama mchango. Kwani Allah, Aliye Mtukufu, Anaibariki riziki ya yule anayetoa ahadi kwa ajili ya Allah, kutoka sasa na kuendelea…. Basi kila mmoja afunge ahadi na Allah Mtukufu, kwamba bila shaka atatoa kiasi fulani kama mchango wake bila kukosa. Mtukufu Mtume wetu Muhammad s.a.w. alipo waomba masahaba watoe mali sawa na uwezo wao alitaka kujua nani atatoa kiasi gani. Tunaelezwa ya kwamba Hadhrat Abu-Bakar r.a. akaleta mali yake yote aliyikuwa nayo. Naye Hadhrat Umar r.a. akaleta nusu mzima ya mali yake. Ndipo mtukufu Mtume s.a.w. akasema Hii ndiyo tofauti katika Daraja zenu. Katika zama hizi kuna watu ambao hawajui kuwa kuna ulazima wa wao kutoa msaada katika dini,ili hali wenyewe wanishi maisha ya hali ya juu sana. Kinyume chake kuna mabaniani ambao wanatoa Malaki ya fedha ili kuendesha viwanda, wakati huo huo wanajenga majengo makubwa y aibada kwa gharama kubwa. Sisi tumetakiwa kutoa michango miepesi sana vipi tushindwe?

Suala la kutoa michango liwe ni makubaliano kati ya mja na Mola wake Mwenyezi Mungu makubaliano ambayo lazima yatekelezwe. Kwa vyovyote kukosa kutekeleza makubaliano hayo itakuwa hiyana kubwa. Katika kutoa michango Imani inapanda na kuongezeka. Kwa hiyo wajibu huu wa kutoa michango katika njia ya Mwenyezi Mungu utekelezwe kwa mapenzi na Jazba ……

Malfoozat Jalada la 6 ukrasa wa 38-43.

Kwa kumalizia tunamuomba sana Mwenyezi Mungu, Atie Baraka zaidi na zaidi katika mali zetu na baada ya kupata mali nyingi, Atupe pia moyo wa kutoa katika njia yake. Amin.

TUJIUNGE NA NIDHAMU YA WASIA.

Imamu wetu Mpendwa, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba amedumu kutuhamasisha tujiunge na mfumo wenye baraka wa Wasia. Sikilizeni wito wa ukhalifa. Inukeni na mseme Labbaika (ndio) na muwe miongoni mwa wale ambao kwao Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika kuwa: "Na ninahisi kwamba wale, baada ya kuambiwa mfumo huu wa kimbingu, bila ya kusita, watafanya mpango kwa shauku wa kutoa moja ya kumi ya mali yao katika njia ya Allah, bali wakaonesha shauku kubwa zaidi, Basi hao, kwa hakika, ndio walioweka muhuri kwenye imani yao.

Limetolewa na Katibu wa Idara ya wasia makao Makuu

Nilivyojiunga na Jumuiya Ahmadiyya

Na Abdallah M. Gesabo - Kurutiyange Jamaat

Kwanza mimi nilikuwa Mkristo. Mimi nilikaa katika Ukristo muda mrefu mno. Zaidi ya miaka minne (4) hadi sasa. Hivi sasa nimeamua kuacha Ukristo kwa sababu niliona kwamba mimi mwenyewe sina budi kuyaacha mafunzo ambayo hayana mwongozo. Maana mhubiri alikuwa akihubiri ya kwamba "msifanye uasherati" na mara tu siku mbili zikipita tunamwona ameletwa kanisani ya kwamba alishikwa na mke wa mtu, na huyo huyo ni Mchungaji wa kanisa. Si maajabu hayo! Niliudhika sana moyoni mwangu.

La pili ni kwamba ninapoona katika Torati inaamuru kwamba msile nguruwe wala sungura wala bata na wao hao Mabishop, Mapastor watuamuru kwamba tule. Maana hiyo ni Agano la Kale tunafuata Agano jipya pekee.

La tatu ni kwamba tulikuwa tukiamrishwa kufunga saumu. Na hapo kumbe kuna baadhi ya wengine wetu walikuwa wakienda kula wakati hatupo pamoja. Na tulipokuwa tukifunga wao walikuwa wakiamuru kwamba hakuna mtu yeyote atakula chakula chochote. Mimi nasema ukweli mbele za Mwenyezi Mungu hata nina uthibitisho maana tulikuwa wawili ambao tulikuwa tukivumilia kumaliza saumu ya siku 4, 3, na kuendelea, ambao tulikuwa; 1. Abdallah Moi Gesabo 2. Benisoni Chacha John. Sisi ndio tuliudhiwa na wenzetu maana tuliwashika wakila na kunywa siku moja. Ndipo tukaamua kacha sala zao. Pia tulikuwa tukifunzwa tusiweze kutorosha wasichana kanisani. Hao wachungaji walikuwa wakitorosha. Na sasa nauliza hiyo ni kuhubiria watu ukweli ama ni kutukana neno Mwenyezi Mungu?

La nne ni kwamba hiydini iliniudhi sana na siku moja nilimsikia mwalimu akihubiri juu ya kumuabudu Allah Mwenyewe pekee. Mimi ndipo nikaamua kujiunga na Waislamu wa Ahmadiyya. Nilipojiunga katika Uislamu niliyapata mengi ya kufunja moyo.

Hao Wakristo walipoona ya kwamba nimeachana nao walinijia na mambo mbalimbali wakiniambia kwa nini umejiungaa na Uislamu umeachana na Ukristo huu, na Ukristo huu ndio mambo yote.

Nikawauliza kwani Ukristo mzuri ni upi? Ni kufanya uasherati na kuyafuata mafunzo ya uongo na kubagua Biblia na kuwa mnafuata Agano Jipya pekee na kutupilia mbali Agano la Kale na Torati? Mimi nikawaambia hakika hiyo ni imani iliyokufa maana walikuwa wakifanya mambo yasiyopendeza kabisa. Uasherati, uongo, ufisadi, ukahaba, kusengenya, kuenda katika dansi , kuomba usiku katika pango bila taa wavulana na wasichana.

Wakaniambia kwanza Waislamu wanatembea na majini, wanawaua watu kwa visu, Waislamu wanatoa watu sadaka – yaani wanawachinja, Waislamu hawamuabudu Allah wanabudu Muhammad s.a.w, hawana umoja, vijana Waislamu hawaoi, Waislamu utajiri wao ni wa majini pekee. Kisha wakamtukana Mtume Mtukufu wa Mwenyezi Mungu kwamba aliliwa na mbwa, pia alikuwa akifanya ukahaba katika mama mmoja ambae hawakumtaja jina lake. Nikawauliza hamuoni aibu kumtusi Mtume s.a.w Mtukufu wa Mwenyezi Mungu?

Nikaona hawana ukweli nikaachana nao moja kwa moja. Ndipo mwalimu akaja nikamueleza, akanitia moyo akasema achana nao maana wajitafutia laana, siku ya kiyama wataulizwa.

Sasa natangaza kote duniani kwamba nataka niwe mfano ulio hai katika vijana wa Waislamu kwamba wanaoa. Mimi ni kijana wa Kikuria kutoka nchini Kenya. Pia vijana wengi wa Waislamu wameoa. Vijana wa Waislamu wa Ahmadiyya wote wanaoa wanawake kwa wingi. Hata mwalimu wangu ni kijana anaye mke na watoto wanne. Hivyo ni kwamba Waislamu wanaoa.

Watu wengi wananijia wakisema mimi sitaoa maana nimejiunga katika Uislamu nikiwa kijana mdogo sababu nina miaka kumi na tisa(19). Wanasema heri ningejiunga nikiwa na umri wa miaka arobaini (40) na mimi nawaambia la hasha! Sivyo! Mimi hakika ni mfano ulio hai kote duniani kwamba nitaoa nikiwa katika Islam na jamii yangu itakuwa ya uislamu pekee. InshaAllah

Maana mwalimu wangu amenifunza imani iliyo kamili. Na yeye amenifunza nimeweza kuielewa maana ya saumu na maana ya Uislamu, sasa nimeijua sina shaka kamwe. Nakufahamisha mwalimu wangu ni Yusufu Gesonko ambaye anaifanya kazi hii ya Mwenyezi Mungu hapa nchini Kenya. Tawi ni Kehancha, kijiji ni Kurutiyangena mimi ni mwanajumuiya wa Ahmadiyya Muslim Jamaat.

Namalizia nikisema wanajumuiya wote wa dini hii ya Mwenyezi Mungu Ahmadiyya ulimwenguni kote mniombee ili nizidi kutembea katika mwanga huu nilionao wa Kiislamu. Namalizia nikisema kwa Waislamu wote ulimwenguni Assalamu Alaykum Warahmatullah Wabarakatu.

Khalifa Mtukufu atangaza mwaka wa 61 wa Waqfe Jadid

Kutoka uk. 12

(AS) anasema, ninaangalia upendo na utii wa Jumuiya yangu kwa mshangao kwani walio masikini kabisa miongoni mwao, kama vile Mian Jalal-ud-Din, Khair-ud-Din na Imamu-ud-Din wa Kashmir, ambao wanaishi karibu na kijiji changu; hawa na ndugu watatu walio masikini, ambao pengine kipato chao kwa siku ni annas tatu au nne, lakini, wanajitolea Chanda kila mwezi. Masihi Aliyeahidiwa (AS) anasema zaidi, pia ninashangazwa kuhusiana na utii wa marafiki zao, Mian Abdul Aziz, ambaye ni mkusanya mapato. Ingawa yu masikini, siku moja alitoa rupia mia moja na akasema kwamba ninataka hii itumike katika njia ya Mungu'. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema, Inawezekana mtu huyu masikini amedunduliza rupia hizi mia moja kwa miaka kadhaa, lakini, pendo lake kwa Mungu limepenyeza nafsini mwake ladha ya kujipatia radhi ya Mungu.'

Kwa Msaada wa Allah Mwenyezi, hili linaweza kuonekana miongoni mwa Jamaat ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s) hata leo hii. Allah Mwenyezi amepenyeza kwenye Jamaat ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s) uelewa ule wa mfumo huu wa kujitolea, ambao kama nilivyosema, haujapenyezwa kwa mwingine yeyote. Leo hii, sawa na utamaduni wa kutangaza kuanza kwa mwaka mpya wa Waqf-e-Jadid katika hotuba ya kwanza ya Januari, nitasimulia matukio ya kukuza imani kuhusiana na kujitolea kifedha katika Waqf-e-Jadid na jinsi gani Allah Mwenyezi, kutokana na kujitolea kwao, Amewabariki katika dunia hii, ambayo mwishowe imekuwa ndio njia ya kuimarisha imani yao. Amir Sahib wa Bukina Faso anaandika kwamba Khuddam wanaoishi karibu na Jamaat ya Kari walifanya kazi ya kuchimba kwa pamoja ili kutandaza nyaya za umeme kwa kiasi cha Faranga CFA milioni moja ambazo ni sawa na takribani pauni za uingereza elfu moja mia mbili na hamsini (Shilingi za Kitanzania milioni nne) walizitoa hizo kwenye Chanda Waqfu Jadid. Hivyo, hii ndio ladha ambayo, kama nilivyosema, haiwezi kuonekana nje ya Jumuiya ya Ahmadiyya leo hii.

Hudhur (atba) alielezea matukio mengi ya kukuza imani kuhusiana na jinsi Allah Mwenyezi Alivyoimarisha imani ya vijana na watoto kwa kupitia Baraka za Chanda, idadi ya watu walioona kwamba hali yao ya kifedha imeimarika walipojitahidi kushiriki katika Chanda, ingawa wakiwa katika hali duni kabisa (ufukara). Bibi mmoja alitoa Chanda mali pekee aliyonayo, kuku, na jinsi gani Allah Adhiim aliiondolea famila yake matatizo mengi magumu. Kwa kudumu katika kutoa Chanda, wanafunzi wamekuwa wakipata mapato wasiyoyategemea, walio na maradhi ya muda mrefu wamepata afya njema na wale waliozama chini ya dimbwi la madeni, wakapata raha katika hali ya kifedha. Wale, ambao wakawa wanatoa Chanda bila kukoma, waliona mazao yao yakiongezeka kwa kiasi kikubwa sana, biashara zao zikawa na mafanikio zaidi na kazi zao zikawa zinalipa zaidi na kutosheleza.

Wale waliofikia ufukara wa kutisha pia walijitolea kifedha na kisha Mungu Mwenyezi Akawajaalia kwa njia zenye shani na Akaimarisha imani zao. Hudhur (atba) pia alitoa baadhi ya mifano ya kwamba wale wanaolipa Chanda, Mungu Analinda mali zao kwa njia ya ajabu dhidi ya moto ambao uliunguza mashamba yote ya jirani zao, mwanafunzi mmoja ambaye alilipa Chanda pamoja na kuwa katika hali ngumu, alitunukiwa udhamini nzuri wa masomo na mtu mmoja alitoa taarifa kwamba mshahara wake uliongezeka bila kutegemea baada ya kulipa Chanda. Watu wanajitolea sana mno katika Chanda, kibarua mmoja ambaye anaishi kwenye chumba cha kupanga, aliuza friji yake ili alipe michango katika Chanda, msichana mmoja alisisitiza kwamba baba yake azitoe katika Chanda fedha ambazo amekuwa akizidunduliza kwa ajili ya kumnunulia viatu vya masika. Alisisitiza kulipa Chanda Waqfu Jadid na akasema, viatu vinaweza kununuliwa baadae lakini lipia Chanda sasa.

Haya ni matukio machache niliyoyaeleza ambayo sio tu yanadhihirisha kujitolea kifedha kulikofanywa kwa ajili ya imani, lakini pia ni uthibitisho wa ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) na Jumuiyya ya Ahmadiyya, na ukweli kwamba imeanzishwa na Mungu Mwenyezi. Ninamuomba Mungu Mwenyezi Awawezeshe Wanajumuia waongezeke kiimani na kiitikadi na ninaomba waendelee kuongezeka katika kujitolea kwao ili kupata radhi ya Mungu Mwenyezi. Sasa nitataja kujitolea kifedha kulikofanywa na Jamaat mbalimbali katika mwaka uliopita kuhusiana na Waqf-e-Jadid na pia kuonyesha nafasi zao.

Kwa Baraka za Mungu Mwenyezi, mwaka wa 60 wa Waqf-e-Jadid umefikia ukingoni na kuanzia tarehe 1 Januari 2018 mwaka wa 61 umeanza. Jumuiya ya Ahmadiyya duniani kote imejitolea jumla ya Pauni za Kiingereza milioni 8.862 katika mfuko wa Waqf-e-Jadid. Hilo ni ongezeko la paundi 842,000 kulinganisha na mwaka uliopita. Baada ya Pakistani, ambayo daima inabaki kwenye nafasi ya kwanza, nafasi kumi za juu za nchi katika sehemu zilizobaki za dunia kuhusiana na jumla ya mchango ni kama ifuatavyo:

Ya kwanza ni Uingereza, ya pili ni Ujerumani (lakini katika Tahrik Jadid nafasi zao zilikuwa ni kinyume cha hivyo) kisha ya tatu ni Marekani, ya nne ni Canada, ya tano ni India, ya sita ni Australia, ya saba ni nchi fulani ya Mashariki ya kati, ya nane ni Indonesia, ya tisa ni nchi fulani ya Mashariki ya kati na ya kumi ni Ghana. Ghana imefanya maendeleo makubwa sana mwaka huu.

Kwa kuangalia sarafu ki nchi, nchi zilizofanya ongezeko la maana kwa kulinganisha na mwaka uliopita: Canada ni ya kwanza kwenye orodha, wamefanya maendeleo mazuri. Miongoni mwa nchi za Afrika Nigeria imefanya maendeleo mazuri ikiwa na ongezeko la 83%, Mali imepata 55%, Sierra Leone 45%, Cameroon 45% Ghana 25%, yaani zote hizi ni ongezeko katika makusanyo kulinganisha na mwaka jana.

Kuhusiana na washiriki, na la muhimu ni kwamba washiriki lazima waongezeke, kwa Baraka za Allah zaidi ya watu milioni 1.6 wamechangia mfuko wa Waqf-e-jadid. Kumekuwa na ongezeko la washiriki 268,000. Kwa muktadha huu, Nigeria imesimama ya kwanza, kisha Sierra Leone, Niger, Benin, Mali Cameroon, Ivory Coast, Senegal, Burkina Faso, Gambia, Guinea-Bisau, Kenya, Tanzania, Zimbabwe. Wote wamefanya kazi ya maana kuhusiana na hili.

Kuhusiana na Chanda Balaghan, katika sehemu kama Pakistan na Canada kuna aina mbili za Chanda; Atfal na Balaghani (waliobaleghe), lakini katika mgawanyo huu Australia pia walishiriki. Katika Pakistan, watatu wa kwanza katika Balaghaani ni: Nafasi ya kwanza ni ya Lahore, ya pili ni ya Rabwah, ya tatu ni Karachi. Kwa kutizama wilaya nafasi ilikuwa kama ifuatavyo: Islamabad imekuwa ya kwanza, kisha Rawalpindi, Sargodha, Gujrat, Umarkot, Hyderabad, Mirpur Khas, Dera Ghazi Khan, Kotli Azad Kashmir na Quetta. Jamati kumi za kwanza kuhusiana na jumla ya makusanyo ni kama ifuatavyo: Jiji la Islamabad, Gulshan Iqbal Karachi, Smanabad Lahore, Mji wa Rawalpindi, Azizabad Karachi, Delhi Gate Lahore, Mughalpura Lahore, Mji wa Sargodha na mji wa Dera Ghazi Khan. Jamaat tatu za kwanza kwa Atfal ni kama ifuatavyo: ya kwanza ni Lahore, nafasi ya pili ni Karachi, na nafasi ya tatu ni Rabwah. Kiwilaya nafasi ni kama ifuatavyo: Sargodha, Rawalpindi, Gujrat, Faisalabad, Hyderabad, Narowal, Dera Ghazi Khan, Kotli Azad Kashmir, Sheikhpura, Badin.

Kwa Jamati kubwa kupita zingine ndani ya Uingereza kumi za kwanza ni kama ifuatavyo: Kwanza ni Worcestor park, pili ni Masjid Fazl, tatu ni Birmingham South, nne ni Gillingham, tano ni Birmingham West, sita ni New Malden, saba ni Glasgow, nane ni Islamadab, tisa ni Putney na kumi ni Hayes. Kimikoa nafasi ni kama ifuatavyo: Ya kwanza ni London B, ya pili ni London A, kisha Midlands, North East, Middlesex, South London, Islamabad, East London, North West, Hertfordshire na Scotland.

Huko Marekani nafasi kumi za kwanza ni kama ifuatavyo: Ya kwanza ni Silicon Valley, kisha Seattle, Detroit, Silver Spring, Central Virginia, Boston, Los Angeles East, Dallas, Houston North na Orwell. Kwa kuangalia makusanyo huko Ujerumani Imarati tano za kwanza ni kama ifuatavyo: Hamburg, Frankfurt, Wiesbaden, Gross-Gerau, Morfelden Walldorf. Kwa kuangalia jumla ya makusanyo Jamaat (huko Ujerumani) kumi za kwanza ni kama ifuatavyo: Rodermark, Neuss, Mahdiabad, Nidda, Freiburg, Koblenz, Florsheim, Weingarten, Pinneburg na Langen.

Nafasi za Jamati za Canada kuhusiana na jumla ya makusanyo ni kama ifuatavyo: Vaughan, Calgary, Peace Village, Brampton, Vancouver, Mississauga. Jamati kumi kubwa ni kama ifuatavyo: Durham, Edmonton West, Saskatoon South, Windsor, Bradford, Saskatoon North, Montreal West, Lloydminster, Edmonton East na Abbostford. Jamaat tano maarufu kwa Daftar Atfal ni kama ifuatavyo: Durham, Bradford, Saskatoon South, Saskatoon North na Lloydminster. Imarati tano maarufu kwa Daftar Atfal ni kama ifuatavyo: Peace Village, Calgary, Vaughan, Vancouver, Vesten.

Huko India, nafasi kimajimbo ni kama ifuatavyo: Kerala, Jamu Kashmir, Telangana, Karnataka, Tamil Nadu, Odisha, West Bengal, Punjab, Uttar Pradesh, Maharashtra. Kwa kuangalia jumla ya makusanyo katika Jamati huko India nafasi ni kama ifuatavyo: Calicut, Hyderabad, Pathapiriyam, Qadian, Kolkata, Bangalore, Kannur Town, Pangadi, Karvalai, Karunagappalli.

Jamaat kumi kubwa za Australia ni kama ifuatavyo: Castle Hill, Brisban Logan, Marsden Park, Melbourne Long Warren, Berwick, Pezith, Plumpton, Black Town, Adelaide South, Canberra. Jamaat maarufu za Australia kuhusiana na Daftar Atfal ni kama ifuatavyo: Brisbane Logan, Pezith, Brisbane South, Melbourne, Brewick, Adelaide South, Melbourne Long Warren, Plumpton, Castle Hill, Marsden Park na Druitt.

Ninamuomba Mungu Mwenyezi Awajaalie mali nyingi na Baraka kwa wale wote waliochangia na Awabariki kwa kiwango kikubwa. Ninaomba imani yao na utii wao uongezeke, na ninaomba kila mmoja atafute radhi ya Mungu Mwenyezi kwa kupitia kila tendo lake na kauli na vitendo.

Baada ya sala nitaongoza sala ya jeneza ambayo iko hapa leo, ambayo ni ya Ali Gohar Munawar, mtoto wa kiume wa Wajih Munawar Sahib wa Aldershot, Uingereza. Alikuwa akisafiri kuelekea Ujerumani akiwa na familia yake. Walipokaribia Cologne walipata ajali ya gari tairi lilipopasuka. Mama yake alikuwa akiendesha gari hilo. Amefariki akiwa na umri wa miaka mitano. Inna Lillaahi wa inna Ilaihi raajiuun. Kwa Baraka za Allah, wazazi wameubeba msiba huu kwa subira sana, na hasa mama. Watoto hawana kosa na bila shaka Mungu Mwenyezi Anawawezesha watoto kuingia peponi mara moja. Ninamuomba Allah Awajaalie wazazi subira na uimara na Awajaalie fidia bora kabisa. Amin

Lajna Imaillah na Wajibu Wetu

Na Farzana Rafique
Katibu Lajna Taifa

Akina mama ndio wanaoonyesha muongozo muhimu kwa watoto. Tangia mtoto anazaliwa anakuwa jirani na mama mpaka anapopata fahamu ya kutambua mabaya na mazuri katika ulimwengu. Mama mwenye maadili mazuri anamfanya mtoto kuwa kiongozi bora, muumini bora wa Mwenyezi Mungu na mtu wa faida kwa jamii yote kwa ujumla.

LAJNA "wanawake watumishi wa Mwenyezi Mungu" "maids of Allah". Ni kikundi cha wanawake wa Kiahmadiyya kuanzia umri wa miaka 15 na kuendelea. Kiliundwa mwaka 1922 na Mirza Bashir-ud-Din Mahmood Ahmad, Khalifa Mtukufu wa 2 r.a; ambaye alisema "jitihada ya wanawake pamoja na wanaume ni muhimu sambamba kufikia malengo ya kuumbwa kwetu" Kikundi hiki kilianza ili kuwapa akina mama sauti katika mambo ya utawala na kiwango cha uhuru. Ni kikundi kikubwa ukilinganisha na vikundi vingine kama Ansarullah, Khudam zikiwa baadhi ya vikundi vingine.

Lengo kuu la Lajna Imaillah ni kuongeza uelewa kati ya wanawake Waahmadiyya kuhusu umuhimu wao na majukumu yao katika Jumuiya, wakati huohuo wakitimiza majukumu yao ya kijamii ikiwemo utu, kuishi vizuri katika mazingira yao, kusaidia jamii iliyowazunguka na kukuza kizazi chema kijacho. Wanawake wa Kiislamu wa Kiahmadiyya wana kamati yao ya utendaji ambayo inasimamia mipango ya fedha, elimu, afya, huduma za jamii, uchapishaji nk. Sadr wa Taifa (Rais) anayechaguliwa na Lajna wenyewe ndiye kiongozi anayesimamia utekelezaji wa wajibu wa kila kamati; kamati hii inaitwa Majlis Amila Taifa. Tanzania tandhim hii ilianza takriban mwaka wa 2000, Sadr wa kwanza wa kina mama ni Mama Radhia Kaluta. Majlis Amla ya sasa ina wanachama 15 na kila mwezi mara 1 inafanya kikao ili kupanga vizuri mikakati yao na kufuatilia kama majukumu na malengo yametimia kama kuna mapungufu yarekebishwe. Majlis Amila Taifa ina majukumu ya kuandaa. Ijtimaa ni mkutano wa mwaka wa Lajna, ambao unakusanya Lajna na Nasrat (ambao ni kikundi cha watoto wa kike chini ya umri wa miaka 15). Hii inawapa Lajna faida ya kujifunza Neno la Mungu, kuongeza imani, kubadilisha mawazo, kujiendeleza kielimu, pia kunakuwepo michezo, sehemu ya afya bora. Majlis imefanya ziara ya kutembelea Lajna mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora hadi vijijini katika mikoa hii. Pia semina za mafunzo imefanyika katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Morogoro na Dutumi. Kambi kwa ajili ya Nasrat(watoto wa kike chini ya miaka 15) imefanyika mwezi Disemba, hii inasaidia kuelimisha watoto kidini, jinsi ya kuishi vizuri katika jamii, kutimiza wajibu wao nk. Shukrani inaenda kwa familia za Lajna wanaojitolea, bila ya msaada wao ni vigumu kutimiza wajibu, na pia Allah Aendelee kubariki Lajna kwa ujumla ili wawe watiifu kwa Khilafat na kusaidia Jumuiya kwa pamoja kwa kazi zao za kujitolea. Allah Atuwezeshe. Amin.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Jum I - Jum. II 1439 AH | FEBRUARI 2018 | Tabligh 1397 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat 'Adil bin Hatim r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Jikingeni na Moto walau kwa (kutoa katika njia ya Allah) kipande cha tende. (*Bukhari*).

Khalifa Mtukufu atangaza mwaka wa 61 wa Waqfe Jadid

Mchango wa dunia wazidi £mil. 8, Tanzania yafanya vizuri kwa idadi ya wachangiaji

Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 05/01/2018, Hadhrat Amir-ul Muminiin, Khalifatul Masih V a.t.b.a. alizungumzia juu ya Kujitolea kifedha na Waqfe Jadid 2018.

Baada ya Tashahhud, Taa'udh na Surat Fatihah Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema:

Katika Qur'ani Tukufu, tunaona katika maeneo mengi kwamba, uangalifu wa waaminio umekuwa ukielekezwa kwenye kujitolea kifedha.

Kwenye sehemu moja, Allah Mwenyezi Anasema, 'wa maa tunfiquu min khairin fa li-anfusikum' yaani 'Na mali yoyote mtakayotoa, basi ni (faida) kwa nafsi zenu,. (2:273) Pamoja na hili, sifa ya waaminio pia imeelezwa kuwa hutumia tu ili kupata Radhi ya Allah. [Qur'ani Tukufu] inasema kwamba, *'wa maa tunfiquuna illabtighaa'a wajhillah'* yaani '... hawatumii ila kutafuta Fadhili za Allah'.

Kwa hiyo, ni bahati nzuri kwa wale watu ambao hutumia mali yao katika njia ya Allah Mwenyezi tena kwa muelekeo huu. Allah Mwenyezi Hahitaji mali yoyote kwa manufaa Yake. Maana ya kweli ya matumizi kwa ajili ya Allah ni kutumia kwa ajili ya kufaidisha viumbe vyake na kwa kuifanya dini Yake ishinde dini zote.

Wakati akimnukuu Allah Mwenyezi, Mtukufu Mtume (s.a.w) alisema (katika Hadithi Qudsi) kwamba, 'Ewe mwana wa Adamu! Weka mali yako kwangu na usiwe na shaka nayo kwa sababu haiwezi kudhurika kwa kuangamizwa na moto wala kuhilikishwa kwa maji, wala kuibiwa na mwizi. Nitairudisha yote, hazina ambayo unaiweka kwangu, itakufaa siku ambayo utakuwa na uhitaji nayo sana.' Hii ina maana kwamba chochote tunachokitoa kwa ajili ya Allah, kinawekwa katika akaunti zetu wenyewe. Na tutakapokihitaji, Allah Mwenyezi Atakirudisha.

Vivyo hivyo, inasemwa katika maelezo ya kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w) alisema: "Siku ya Kiyama, wale wanaotumia katika njia ya Allah wataendelea kuwa chini ya kivuli cha mali waliyoitumia katika njia ya Allah hadi hukumu itakapokuwa imefikia mwisho. ' Hata hivyo, Mtukufu Mtume (saw) amesema pia kwamba Allah Mwenyezi haipendi mali isiyofaa (ya haramu.)

Hivyo, tunapaswa kukumbuka daima kuwa mali yetu lazima iwe safi. Masahaba wa Mtukufu Mtume (saw) wote matajiri na maskini, waliweza kupata na kutoa sadaka kwa kufanya kazi ngumu na kufanya kazi tu ili kupata Radhi ya Allah Mwenyezi. Kuna maelezo fulani juu ya Hadhrat Abu Bakr Siddiq (ra) kwamba alipoukubali Uislamu, alikuwa na akiba ya arobaini elfu ya Ashrafis [sarafu] mbali ya biashara na mali yake. Ikiwa tunalinganisha Ashrafi ya dhahabu ya wakati huo kwa thamani yake leo hii, labda itakuwa sawa na paundi za kiingereza kumi na moja au kumi na mbili milioni.

Halafu, sisi pia tunaona hili miongoni mwa masahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Tunasikia matukio ya kujitolea ya Hadhrat Khalifat-ul-Masih I (ra), ambaye alijitolea pasipo kifani kila wakati Masihi Aliyeahidiwa a.s alipoitisha kujitolea. Alikuwa daktari kwa taaluma na mtumishi wa umma. Alikuwa mwenye ukwasi na alipata mapato makubwa.

Masihi Aliyeahidiwa (as) amemjumuisha yeye kuwa miongoni mwa wanafunzi wake kumi na wawili. Hadhrat Musleh-e-Mau'ud anasema kwamba kujitolea kwake kulikuwa kwingi sana kiasi kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s alimpa heshima [akisema] umejitolea mara nyingi sana kwa ajili ya Jama'at hii ambapo huna tena haja yoyote ya kujitolea zaidi.

Kwa hali yoyote ile, hawa walikuwa watu ambao wakijitolea. Hata hivyo, licha ya kupokea heshima hii, hakuacha kujitolea. Badala yake, aliendelea kufanya hivyo. Wakati Masihi Aliyeahidiwa (as) aliposhtakiwa katika kesi ya Gurdaspur, Masihi Aliyeahidiwa a.s aliomba (kujitolea kifedha) kwa marafiki zake kutokana na gharama zilizoongezeka.

Khalifa Rashid-ud-Din Sahib, alipopokea mshahara wake na ikatokea kwamba siku hiyo ndipo alipopata kujua kuhusu ombi hilo la Masihi Aliyeahidiwa a.s, basi alipeleka mshahara wake wote kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s, ambao ulikuwa rupia mia nne na hamsini kwa wakati huo ni kiasi kikubwa, sawa na mamia ya maelfu leo hii. Rafiki yake alimwambia kuwa angepaswa kuzingatia kuhifadhi mahitaji ya nyumbani na familia yake. Juu ya hayo alijibu kwamba ikiwa Masihi wa Mungu anasema kwamba hizi zinahitajika kwa ajili ya dini, basi ni sababu gani tena inifanye kuhifadhi kitu? Hivyo, kama hizi zinahitajika kwa ajili ya dini, basi kila kitu kitakwenda kwenye dini.

Halikadhalika, Masihi Aliyeahidiwa (AS) pia ametaja kwa namna ya upendo sana kujitolea ki mali kulikofanywa na baadhi ya Waahmadiyya wake masikini. Masihi Aliyeahidiwa

Endelea uk. 11

Kutoa Katika Njia ya Mwenyezi Mungu

Na Mwandishi Wetu, Dar es Salaam

Ndugu waheshimiwa, Assalam alaikum warahmatulahi wabarakatuhu. Ama ba`ad mada nilivyo pewa kuzungumzia inahusu ''kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu '' Tunapotoa mali katika njia ya Mwenyezi Mungu tunatarajia (a) kupata radhi ya Mwenyezi Mungu, (b) Tunafanya ibada ya mali, na wakati huo huo (c) Tunachangia maendelea ya nchi.

Ieleweke kwamba mali yeyote tunayoipata kwa hakika ni amana tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kwa hiyo Mwenyezi Mungu Mwenye amana hiyo Anataka mali itumike kwa namna ya kumlidhisha Yeye. Ikiwa ni pamoja na kuwasaidia wenye shida. Kurani tukufu inatukumbusha kwamba:- ''Nakatika mali zao imo haki ya aombae na ajuzuiaye '' (15:20) kwa mujibu wa aya hii ni wazi kwamba sehemu ya masikini ipo katika mali za matajiri. Kwa hiyo matajiri wanalimbikiza mali zao na kukiuka agizo lililotajwa hapo juu,.Pamoja wanakuwa wanavunja Amri ya Mwenyezi Mungu, lakini pia wanakuwa wasababishaji wa fitina, vurugu na hata vita.

Ni kweli kwamba binadamu sisi sote tupo sawa mbele ya muumbaji wetu. Tunayo haki sawa katika kumiliki mali, lakini kila mmoja hupata sehemu ya mali yake sawa na kipaji, akili na juhudi yake katika kutafuta mali hiyo. Kutokana na tofauti iliyopo juu ya vipaji vyetu katika kutafuta mali, ndio maana Mwenyezi Mungu Amewasisitizia wenye uwezo mkubwa kifedha waitambue haki ya waombao ambayo ipo katika mali zao. Kwa upande mwingine wasio na uwezo wameshauriwa kushika subira bila kuikodolea macho mali ambayo nao bado hawajaipata. Mara nyingi wizi na ujambazi unafanyika kwa sababu; aidha wenye uwezo wamenyima kutoa haki za wasio na uwezo, au wasio na uwezo wamekosa subira ndipo wakapora mali ya wengine. Kwa hiyo matajiri wenye uwezo na masikini wasio na uwezo kama wote watazingatia nasaha hizi njema zilizotolewa na Allah kwenye vifungu tulivyotaja hapo juu, ni wazi matokeo yake yatakuwa kwamba wizi na ujambazi utatoweka katika jamii yetu, nayo jamii itabaki katika amani na utulivu. Ndani ya Kur`an tukufu kuna aya nyingi zinazoeleza umuhimu wa kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hapa chini tunarejea aya mbili:-

" Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu, ni kama mfano wa punje moja itoayo masuke saba, katika kila suke punje mia na Mwenyezi Mungu Humzidishia Amtakaye na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua, (2:262). Pia tunasoma katika Kur`an Tukufu " Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Mwenyezi Mungu na kujiimarisha wenyewe, ni kama mfano wa Bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta matunda yake mara mbili, na kama haifikiwi na mvua kubwa basi mvua ndogo (huitoshea); na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda (2:266)

Baada ya kutoa maelezo mazuri juu ya ubora wa kujitolea katika njia yake, Mwenyezi Mungu Ametoa onyo pia, kwa wanaofanya ubahili bila kutoa mali zao katika njia Yake. Mwenyezi Mungu subuhanahu wa Taala Anasema ndani ya Kur`ani Tukufu:- " Wala wasione wale ambao wanafanya ubahili katika yale Aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika fadhili zake kuwa ni bora kwao; la, ni vibaya kwao,watafungwa kongwa za yale waliyofanyia ubahili siku ya kiyama"(3:181). Sehemu nyingine tunasoma:-"na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, basi wape habari za adhabu iumizayo. Siku (mali yao) itakapotiwa joto katika moto wa Jahannamu na kwayo vitachomwa vipaji vya nyuso vyao na mbavu zao na migongo yao; haya ndiyo mliyoyakusanyia nafsi zenu, basi onjeni adhabu ya yale mliyoyakusanyia nafsi zenu, basi onjeni adhabu ya yale mliyokuwa mkikusanya "(9:34-35). Hayo ndiyo magombezo makali ambayo Mwenyezi Mungu Ameyatoa dhidi ya wale ambao hawataki kujitolea katika njia yake.

Sasa tuangalie Mtume wetu Mtukufu Muhammad s.a.w alisemaje juu ya jambo hili. Abu Huraira (r.a) anasimulia kwamba Mtume s.a.w alisema, "kila asubuhi watu wanapoamka, wapo Malaika wawili wanaoshuka. Mmoja wao husema Ee Mola wangu, atoae mpe zaidi; na wa pili husema Ee Mola wangu, azuiaye mali Uangamize mali yake (Bukhari na Muslim). Sawa na maelezo ya hadithi hii ni wazi kwamba, mwenye kulimbikiza mali yote wala hataki kutoa sehemu ya Mwenyezi Mungu ili iwasaidie walengwa wanao husika, basi Malaika huiombea maangamizo mali hiyo, na matokeo yake ni kwamba mali inafilisika. Tumeshuhudia mara nyingi watu ambao walikuwa matajiri wakubwa, lakini kwa kosa kuzingatia jambo hilo baadaye wakaja kuwa masikini wa kutupwa. Ifahamike basi kwamba kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu kifedha kunatia baraka mali, nayo inakuwa chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Akifafanua jambo hilo Mwanzilishaji mtukufu wa Jamaati Ahmadiyya, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. amesema:- Mnapotoa mali zenu katika njia ya Mwenyezi Mungu, msidhani kwamba mnamfanyia hisani Mwenyezi Mungu la, bali ukweli ni kwamba Mwenyezi Mungu Anakufanyieni hisani kubwa kwa kuwapa hiyo nafasi ya kutoa mali zenu katika njia yake;

Kuna vipengele vingi vya kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu kifedha, na mtu anapojitolea kupitia kipengele chochote katika vipengele hivyo, anahesabiwa kuwa ametoa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hapa chini ninataja baadhi tu ya vipengele hivyo:-

1 ZAKA: Ni sehemu ya arobaini kwa moja (1/40) ya mali ile yenye nisabu kamili iliyo pitiwa na mwaka mzima inabidi itolewe zaka. Shabaha ya mchango huu ni kwamba mali isijilundike katika mikono ya matajiri wachache na hali kuna masikini wengi hohehahe. Kwa kuzingatia umuhimu wa kutoa Zaka utakuta ndani ya Kur`ani Tukufu mara nyingi Mwenyezi Mungu kila alipoagiza kusimamisha Sala, akaagiza pia na kutoa Zaka. Hii inamaana kwamba mtu anaposali huwa anatimiza haki ya Mola wake; na kwakutoa zaka mtu anatimiza haki ya viumbe wa Mwenyezi Mungu.

2 SADAKA: Ni kiasi chochote cha mchango unaotolewa kwa madhumuni ya kujikinga na mabalaa kama vile alivyosema Mtukufu Mtume s.a.w.

"Kwa hakika sadaka inazuia mabalaa."

3 MAHITAJI YA UMMA: Ni aina zote za michango inayotolewa kwa madhumuni ya kutoa huduma za Jamii. Michango hiyo inahesabiwa kuwa inatolewa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Ndio kusema tunapo changia ili kuboresha huduma ya Afya elimu, na Mawasiliano n.k. basi michango kama hiyo inatambuliwa kuwa inatolewa katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa manufaa ya viumbe

Endelea uk. 10